

# SALAT

Kitabu cha Sala ya Kiislam

Mfasiri: Jamil R. Rafiq

JUMUIYA YA WAISLAMU  
WAAHMADIYYA  
TANZANIA

# **SALAT - Kitabu cha Sala ya Kiislam**

**Mfasiri: Jamil R. Rafiq**

© Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania

Chapa ya mara ya Kwanza (Kiingereza) 1994

Chapa ya mara ya Pili (Kiingereza) 1996

Chapa ya mara ya Kwanza (Kiswahili) 2000.

Nakala 5000

Chapa ya mara ya Pili (Kiswahili) 2008

Nakala 2000

**Kimeenezwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya**

**P. O. Box 376**

**Dar es Salaam.**

**Tanzania**

**Kimechapwa na:**

**Ahmadiyya Printing Press,**

**Dar es Salaam,**

**Tanzania.**

## **YALIYOMO**

1.	Umuhimu wa Sala .....	1
2.	Kusali ni Faradhi. ....	2
3.	Nyakati za Sala .....	6
4.	Sharti za Sala .....	8
5.	Udhu. ....	9
6.	Mambo yanayotangua udhu. ....	13
7.	Kuoga. ....	15
8.	Adhana. ....	17
9.	Kukusanya Sala. ....	23
10.	Njia ya Kusali .....	25
11.	Sala ya Mtu peke yake. ....	42
12.	Sala Pamoja na Jamaa. ....	42
13.	Mambo mengineyo ya kuzingatia .....	44
14.	Kumkumbuka Allah baada ya kumaliza Sala. ....	47
15.	Aina ya Sala na Rakaa zake .....	50
16.	Sala ya Ijumaa. ....	52
17.	Sikuu za Idi; Fitri na Idil Adh-ha .....	56
18.	Sala ya Witri. ....	59
19.	Sehemu mbalimbali za Sala. ....	60
20.	Mambo yanayovunja Sala. ....	66
21.	Sujuda za Kusahau .....	67
22.	Sala ya Mgonjwa. ....	68
23.	Sala ya Safari. ....	68
24.	Sala ya wakati wa hatari .....	70
25.	Kukidhi Sala. ....	70
26.	Sala ya Tahajjud .....	71
27.	Sala ya Tarawehe. ....	72
28.	Sala ya kupatwa jua na mwezi .....	73
29.	Sala ya kuomba mvua .....	73
30.	Sala ya Istikhaara .....	75
31.	Salatul Hajah .....	76
32.	Sala ya Ishrak .....	77
33.	Sala ya Jeneza .....	79
34.	Orodha ya Istilahi .....	86

## **NENO LA MBELE**

Idara ya Islam International publications Ltd. inatoa huduma isiyi kifani katika uwanja wa uenezaji wa mafundisho sahihi ya Kiislamu, na inashughulika usiku na mchana kutoa vitabu vya kumstawisha mwenye hamu kiroho. Utoaji wa kitabu hiki kiitwacho SALAT - Kitabu cha Sala ya Kiislamu, ni dalili nyingine ya uhakikisho wa shughuli hizo.

Sala katika kila dini huhesabiwa kuwa ndiyo imwezeshayo mtu kuongea na Mungu na kujenga uhusiano naye. Sala kwa kweli ni nguzo ya Pili ya Kiislamu.

Katika ulimwengu wa kisasa wa kuipenda dunia, vitabu vya aina hii vinaweza kuzipatia roho zenye njaa chakula cha kiroho cha kushibisha na kwa hiyo ndiyo hitajio hasa la zama hizi.

Pakiwepo na watu wengine wanaoendelea kusilimu, bila shaka kitabu hiki kinaweza kuwa chombo cha kuwafunza mambo mbalimbali yahusikanayo na Sala. Ingawaje vitabu vingine juu ya Sala ya Kiislamu pia vinapatikana madukani, lakini mara nyingi hivyo havifafanui habari za Sala kwa mapana na mrefu jinsi Kitabu hiki kielezavyo. Zaidi ya kufundisha matamshi na tafsiri ya maneno ya Kiarabu picha kadhaa pia zimechapwa kwa kufafanua na kuonesha jinsi udhu na Sala na matendo mbalimbali ya Sala yanavyofanywa. Hali mbalimbali za mwili ndani ya Sala, kama vile kusimama wima, kuinama, kusujudi na kadhalika hazina budi kuzingatiwa vizuri, ili kusali barabara sawa na sheria, kwani hali hizo zinaleza hali za kiroho za mwenye kusali mbele ya Mungu. Hizo zote kwa hakika zimefundishwa na Mtume s.a.w. kwa kuambiwa na Mwenyezi Mungu.

Sifa nyingine kubwa ya kitabu hiki ni kwamba Sala za Kiislamu za kila namna, faradhi na nafali, zimeelezwa humu; kwa hiyo msomaji hana haja ya kuhangaika kujitafutia vitabu vingine ili kujua Sala za aina mbalimbali za Kiislamu. Kitabu

hiki chamtosheleza. Hata hivyo, kitabu hiki si kitabu cha fik-hi, kwa hiyo masaala ya kifk-hi hayakuelezwa sana humu. Shabaha ya kitabu hiki ni kumfunza mtu namna ya kusali Kiislamu. Kitabu hiki kwa kweli chahitajika wakati huu na yafaa kipatikane katika nyumba ya kila Mwislamu.

Mwenezaji

## **MLANGO WA KWANZA UMUHIMU WA SALA**

Shabaha kubwa ya mwanadamu sawa na dini ya Kiislamu ni kwamba amwabudu Allah. Ndani ya Quran Tukufu, Allah anasema:

**وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّةِ وَالْإِنْسَانَ إِلَّا لِيَعْبُدُونَ**

Na sikuwaumba majinni na watu ila wapate kuniabudu. (51:57).

Ibada inamaanisha utiifu kamili wa maamirisho ya Allah. Mtume Mtukufu s.a.w. alileta ujumbe wa Mwenyezi Mungu na akaeleza amri zote zile zinazohusu dini ya Kiislamu.

Kuna wajibu wa aina tano aliowekewa mwislamu kutekeleza. Mambo hayo matano huitwa nguzo za Islam.

Nguzo ya kwanza inaitwa Kalima Shahada, kushuhudia kwamba hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah, na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allah. Kuamini Umoja wa Allah ndiyo msingi wa Dini ya Kiislamu.

Nguzo ya Pili ndiyo Sala, yaani kusali sawa na njia iliyo-fundishwa katika dini ya Kiislamu.

Nguzo ya tatu inaitwa Zaka, ambayo kila Mwislamu mwenye hali nzuri analazimika kutoa kila mwaka kwa sura ya nakidi (pesa) ama vitu kama vile mazao ama vitu vinginevyo. Zaka inatumiwa kwa mambo mema yaliyoelezwa ndani ya Quran Tukufu.

Nguzo ya nne ni Saumu, yaani kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhanii.

Nguzo ya tano ndiyo Hijja, yaani kuhiji Kaaba Makkah kwa akali mara moja katika maisha.

Miongoni mwa wajibu wote, Islam imekazania sana kusali. Kila Mwislamu analazimika kusali mara tano kila siku. Zaidi ya hiso Sala tano za faradhi kuna Sala nydinge pia za nafali.

Mwislamu anatilia maanani sana maisha yake ya kiroho jinsi

mtu wa kidunia anavyotia maanani maisha ya kimwili. Kama vile hewa na chakula yalivyo mambo ya lazima kwa maisha yetu ya kimwili, ndivyo ilivyo Sala ambayo husaliwa katika sehemu mbali mbali za siku kuwa ni kitu cha lazima, kwa maisha yetu ya kiroho. Bila kusali mtu hawezি kuishi kiroho.

Katika Sala mtu anakuwa katika hali mbalimbali. Pengine anasimama, hali iitwayo Qiyam. Pengine huinama, hali iitwayo Rukuu, pengine anasujudi hali iitwayo Sajdah. Pengine anaketi kwa njia maalum na hali hiyo huitwa Qa'dah. Katika hali hizo mbalimbali maneno maalum yanatamkwa yaliyofundishwa na dini ya Kiislamu. Kwa kuwa maneno hayo yako kwa lugha ya Kiarabu, hivyo kila Mwislamu anapaswa si tu kuyakumbuka kwa ghaibu bali pia kujua tafsiri yake ili mwenye kusali atambue anazungumza nini na Mola wake wakati wa kusali.

## **KUSALI NI FARADHI**

Kusali kwa njia iliyofundishwa ni faradhi juu ya kila Mwislamu mwenye akili timamu aliybalehe. Kwa watoto siyo faradhi kusali mpaka wapate kubalehe. Hata hivyo inahitajika sana kutia bidii katika kuwalea watoto kwa njia bora ili kwamba wapate kutekeleza amri ya kusali sawa na sheria pindi watakobalehe. Kwahiyoo, ni muhimu sana kuwapa watoto mazoezi na mafunzo mapema. Ndiyo maana Mtume s.a.w. aliagiza kwamba watoto wanapokuwa wenyе umri wa miaka saba, wazazi wawasisitizie kusali. Na wasiposali katika umri wa miaka saba wakemewe. (Abu Dawud, Kitabus-Salaat).

Watoto wanapobalehe hapo wanalahimika kusali. Katika umri mpevu hawawezi kulazimishwa na mtu ye yeyote ama Serikali kusali kwa nguvu, kwani Sala inayosalawa kwa nguvu si chochote wala lolote; bali mtu anapaswa asali kwa upendo wa moyo. Hilo lategemea uhusianio baina yake mtu na Mola wake.

Hivyo, ni wajibu wa wazazi kuwalea watoto wao vizuri na kuwaelekeza tangu utoto wao kusali. Isitoshe, wazazi wanapaswa kumwomba sana Allah kwamba Yeye Awajaalie watoto wao upendo wa kusali kila siku barabara sawa na sheria. Lazima msaada wa Mungu utafutwe, kwani jambo lenyewe ndilo kubwa tena la muhimu sana.

Imeelezwa ndani ya Quran Tukufu ya kwamba Hadhrat Ismail a.s. alikuwa anawasihi ahali zake siku zote kwamba wasimamishe Sala daima dawamu.

Tumeona mara nyingi ya kwamba kama wazee wa familia wanasali kila siku barabara, watoto huanza kuwaiga na wanazoea kusali kama kawaida polepole. Hata hivyo, mtoto anapopata umri wa miaka saba anapaswa kufundishwa njia ya kusali sawa na sheria. Anastahili kutiliwa moyo kusimama pamoja nao na kusali; na ikiwezekana ahimizwe kwenda msikitini pamoja nao. Jambo hili litamtilia mtoto moyoni mwake upendo wa kusali na litahifadhi tabia ya kusali katika kizazi kijacho. Mzazi ama msimamizi wa mtoto bila shaka anaruhusiwa kuwa mkali kidogo ikiwa mtoto hasali katika umri wa miaka 10 hadi 12.

Lakini hiyo haimaanishi kwamba mtoto atendewe kikatili ama atandikwe; bali aonywe kiasi anachoonywa asipoenda shuleni. Naam, watoto wanapofikia umri wa miaka 12 wanapaswa kufahamishwa ya kwamba wazazi wao wamekwisha timiza wajibu wao wa kuwafundisha Sala na kuwaelekeza lakini tangu sasa jambo hili la kusali liko baina yao na Mungu wao ambae Atawauliza kuhusu habari hii. Lakini hiyo haina maana ya kwamba sasa watoto wasitolewe mawaiidha ama kuelekezwa au kusihwiwa kusali, kwani kuwatolea mawaiidha kunaendelea maisha mazima ikiwa kuna haja. Ndiyo kusema kwamba kuwatolea ukali na kadhalika kunaishia mtoto apatapo umri wa miaka kumi na miwili. Kama ilivyoelezwa juu, Hadhrat Ismail a.s. alishika desturi ya kuwaelekeza ahali zake kwa upole na upendo maisha yake mazima. Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. aliwatendea watu wa nyumbani mwake waliopevuka

kwa njia hiyo bora. Imesimuliwa ya kwamba yeye alikuwa anawaamsha bintiye Hadhrat Fatima r.a. na mumewe hadhrat Ali r.a. kwa ajili ya Sala ya Alfajiri.

## UMUHIMU WA KUSALI

Imeelezwa katika Quran Tukufu ya kwamba kusali ndiyo sifa maalum ya lazima ya waaminio. Quran tukufu inasema:

ذَلِكَ الْكِتَبُ لَا رَبَّ لَهُ بِهِ هُدًى لِّلشَّقِّيْنِ ۝ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ  
بِالْعَيْنِ وَيُقْسِمُونَ الصَّلَوةَ وَمَنَا سَرَّ زَقْنَهُمْ يُنفِقُونَ ۝

Hiki ni kitabu kikamilifu kisicho shaka ndani yake. Ni mwongozo kwa wamchao Mwenyezi Mungu ambao hukiamini kisichooenakana na husimamisha Sala na hutoa katika yale Tuliowapa. (2:3-4).

Sala inatusaidia kujiondolea mbali dhambi na inatuelekeza siku zote kwa Mwenyezi Mungu na mambo mema, na kwa hiyo inatutakasa hatua kwa hatua. Lakini huo siyo mwisho. Sala inafanya kazi kubwa zaidi kuliko hiyo. Hiyo inamsogeza mtu karibu na Mwumba wake. Mwenye kumwabudu anajaribu kuiga sifa njema za Allah na mfululizo anapata mabadiliko mema kutoka katika hali duni ya kuwa mtu wa dunia na kuwa mtumishi mwungwana na mtukufu sana wa Allah. Quran Tukufu inaeleza sifa hiyo ya pekee ya Sala ikitisemi:

أُتْلُ مَا آتَيْتَ إِلَيْكَ مِنَ الْكِتَبِ وَأَقِمِ الصَّلَاةَ إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَىٰ عَنِ  
الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَلَذِكْرِ اللَّهِ أَكْبَرُ ۝ وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ ۝

Tafsiri: Soma uliyofunuliwa katika Kitabu na usimamishe Sala. Bila shaka Sala huzuia mambo ya aibu na maovu, na kwa yakini kumbuko la Mwenyezi Mungu ni (jambo) kubwa kabisa. Na Mweyezi Mungu Anajua mnayoyatenda. (29:46).

Sala ndiyo dawa kweli iliyothibitishwa kabisa kwa kutakasa moyo na roho. Ni kwa njia ya Sala pekee ya kwamba twaweza kuimarisha uhusiano wetu na Allah. Quran Tukufu inasema:

إِنَّ الَّذِينَ يَتَلَوَّنُونَ كِتَابَ اللَّهِ وَأَقْأَمُوا الصَّلَاةَ وَأَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ  
سِرَّاقٌ عَلَيْهِمْ يَرْجُونَ تِجَارَةً لَّمْ يَعُودُنَّ لِيُوقَهُمْ أَجُورُهُمْ وَرَبِّنِيدُهُمْ  
مِّنْ فَضْلِهِ إِنَّهُ غَفُورٌ شَكُورٌ  
⑦

Tafsiri: Kwa yakini wale wanaosoma Kitabu cha Allah na wanasi mamisha Sala, na katika yale Tulyowapa wanatoa kwa sitri na kwa dhahiri, wanatumai biashara isiyo angamia, ili awape ujira wao sawasawa na kuwazidishia fadhili Zake. Hakika Yeye ni Msamehevu, mwenye shukurani (35:30-31).

Sawa na kauli ya Mtukufu Mtume s.a.w. Sala ni miiraj (upeo) ya maisha ya roho ya mwaminio. Hiyo ndiyo ibada ya hali ya juu kabisa. Mtume s.a.w. tena amesimuliwa kwamba alisema ya kuwa Sala inampatia mwaminio nafasi ya kuongea na Mola wake.

Itambulikane ya kwamba Sala haipotei bure kabisa. Wakati mwingine upendo wa hali ya juu sana wa Mungu unaleta machozi machoni mwa mwaminio. Pengine upendo kiasi wa Mungu hu-jaza moyo furaha kuu ya kiroho. Hali hizo ni alama za kuonesha kwamba Sala iko hai, ina maana hasa na huleta matunda. La sivyo, matendo rasmi ya kidhahiri hayatoshi kumnu faisha mtu. Bali hiyo ni kutii tu amri bila mtu kutia moyo humo. Ndiyo sababu kila mmoja anayenza kusali inapaswa kujiwekea shabaha hii mbele yake ya kujaribu siku zote kwamba Sala yake iwe hai.

Ndani ya Sala zinapatikana desturi zote na madaraja yote ya kudhihirisha unyenyekevu na utii. Wasalio husimama kwa adabu nyuma ya Imam.

Maamuma wote wanaojipanga nyuma ya Imam katika safu wanalahazimika kumfuata Imam katika matendo yake kila anapotoa mwito. Mwito wake wakati wa kila badiliko lake katika Sala ndio tamko la 'Allahu Akbar', isipokuwa Imam anaposimama wima baada ya kuinama (Rukuu), hapo yeye badala ya kusema 'Allahu Akbar' anasema 'sami'allahu Liman Hamidah', maana yake, Mwenyezi Mungu Humsikiliza anayemhimidia. Imam anapotamka hayo, maamuma wote wanasi mama wima wakiacha mikono yao ikinyooshwa mbavuni wakisema 'Rabbanaa wa lakal hamdu'. Hamdan kathiran tayyiban mubarakan fihi.

Uaminifu na unyenyekevu ndio roho ya Sala. Allah anasema:

**قُلْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ۚ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَشُونَ**

Hakika wamefaulu waaminio ambao katika Sala zao ni wanyenyeketu. (23:2-4).

Mtume Mtukufu s.a.w. alisema: hakuna mtumishi wa Allah anayemnyenyeka Yeye isipokuwa Allah Humrufaisha. Hiyo haimaanishi kwamba Mungu Atamnyanya mbinguni na kiliwili chake; bali maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu Anampandisha cheo chake cha kiroho.

Unyenyekevu wa kweli hupatikana kwa kuzingatia rohoni sifa zote za Allah. Utukufu wa Allah unapomdhahirikia mtu, hapo mtu huyo hana budi kuwa mnyenyeketu.

## **NYAKATI ZA SALA.**

Kwa kila Sala katika Sala tano za faradhi kuwa wakati maalum kwa kulingana na hali ya juu.

Wakati wa Sala yaAlfajiri unaanzia pindi kunapopambazuka na kuendela hadi kabla jua halijaanza kuchomoza.

Wakati wa Sala ya Aduhuuri unaanzia jua baada ya kuwa kichwani linapoanza kuteremka.

Wakati wa Sala ya Alasiri unaanzia jua linapomaliza takriban nusu ya safari yake tangu kuanzia kuteremka hadi kuchwa. Nafasi ya kusali Alasiri inamalizika wakati jua linapokaribia kuchwa lakini halijachwa bado. Lakini ni afadhali kusali Sala hii mapema zaidi kabla jua halijaanza kupunguwa mwanga wake sana.

Izingatiwe kwamba kusali kumekatazwa wakati jua linapoanza kucha na wakati linapokuwa sawasawa juu kichwani na wakati linapoanza kuchwa. Pia baada ya kwisha kusali Sala ya Alasiri hakuna ruhusa ya kusali Sala yoyote ya nafali hadi jua lichwe. Vilevile baada ya kusali Sala ya Alfajiri huruhusiwi kusali Sala ya nafali hadi jua litoke barabara.

wakati wa Sala ya Magharibi unaanzia mara baada ya jua kuchwa hadi kupotea ukungu wa jioni. Lakini neno hili limefarsiwa kwa njia mbalimbali na wanasheria mbalimbali wa dini. Mawahabi na baadhi ya wengine ni wakali sana kusisitiza kwamba Sala ya Magharibi lazima isaliwe mara baada ya jua kuchwa. Hao wanasema wakati wa mwisho wa Sala ya Magharibi ndio ambapo mawingu mekundu yanapotea. Lakini wengine wengi wanashika ya kwamba Sala ya Magharibi inaweza kusaliwa hadi kupotea mawingu meupe, yaani hadi mwanga unapopotea moja kwa moja na giza linaingia. Hao wanasema kwamba saa ya Sala ya Magharibi inaendelea kiasi cha nafasi ya saa ya Sala ya Alfajiri kutokea kupambazuka hadi kucha.

Wakati wa Sala ya Isha, walivyoafikiana wataalamu wote wa mambo ya sheria ya dini, ni pindi mwanga unapopotea kabisa na giza la usiku linapoingia. Wengi wamesema saa za Isha zinaendelea hadi usiku wa manane. Lakini wengine tena wanaziendezea saa za Isha baada ya usiku wa manane hadi mtu aende kulala. Hata hivyo, imeonekana ni bora kusali kila Sala mwanzo-mwanzo wa saa zake.

## **SHARTI ZA SALA**

Ziko baadhi ya sharti za Sala ambazo ni hizi zifuatazo:

i. Kunuia Sala: mwenye kusali anapaswa kufunga nia ya Sala kabla hajaanza kusali.

ii. Sala isaliwe katika wakati wake uliowekwa kwa Sala hiyo.

Hata hivyo, ikumbukwe ya kwamba ikiwa mtu hakusali Sala fulani katika wakati wake kwa sababu isiyoeupukika, mtu huyo anapaswa kusali hiyo Sala wakati anapokumbuka Sala hiyo. Naam, asiisali katika nyakati zile zilizokatazwa kusali humo.

Hapo swali lazuka ya kwamba ikiwa nyakati za Sala na kufunga saumu zinazitegema hali mbali mbali za juu zinavyokuwa sambamba na ardhi inavyozunguka, na kadhalika hali tofauti za mwezi, basi kwa njia gani saa za kusali na kufunga saumu zitajulikana kule kwenye pembe za kaskazini na kusini za duni ambako urefu wa usiku na mchana huwa zaidi ya masaa 24?

Zingatieni ya kwamba Mtume Mtukufu s.a.w. akijibu swali al-iloulizwa na sahaba mmoja alisema ya kuwa katika zile sehemu za dunia ambako usiku na mchana ni zaidi ya masaa 24 Waislamu wanapaswa kusali sawa na urefu wa kawaida wa usiku na mchana; yaani katika kila masaa 24 Sala tano zitasaliwa.

iii. Mwenye kusali awe safi kimwili na inavyowezekana kiroho pia. Usafi unamaanisha ya kwamba:

(a). Mwili usiwe na uchafu.

(b). Kama mtu alienda haja ndogo au kubwa ajisafishe barabara kiasi cha kutobakia uchafu ama athari yake.

(c). Baada ya kujamii, bila kujali shahawa imetoka ama hapana. Kadhalika mtu akitokwa na manii kwa njia yoyote iwayo, kama vile katika hali ya kulala usingizi, yamlazimu aoge kikamilifu; kuzisafisha baadhi ya sehemu zake hakutaleta usafi unaotakikana.

(d). Kuoga maji sawasawa ni jambo la lazima kwa mwanamke baada ya damu yake ya hedhi kukatika kila mwezi.

Vilevile baada ya damu ya uzazi kukatika mwanamke anataki-waaoge maji kikamilifu ndipo atahesabiwa safi.

(iv). Mahali pawe safi na mkeka pia uwe safi.

(v). Mwili uwe umefunikwa vizuri wakati wa kusali.

(vi). Waislamu wanatakiwa kuelekea kibla kaaba (kibla) wakisali.

Kibla ndiyo kaaba iliyoko Makka. Nyumba ya kwanza iliyo-jengwa ardhini kwa ajili ya kumwabudu Mwenyezi Mungu.

Waislamu wote popote walipo duniani wanapaswa daima kuelekea kaaba wakati wa kusali. Lakini katika hali ya safari mtu asipotambua kibla kipo upande gani hapo ye ye halazimiki kuelekea kibla. Vilevile kama mtu anashindwa kuelekea kibla kwa sababu ya kuugua sana, hapo pia halazimiki kuelekea kibla. Na kama mtu yuko safarini hali amepanda farasi au yuko katika gari moshi, meli ama ndege, mtu anaweza kusali tu bila kuelekea kibla. Ikiwezekana asali akielekea upande ule ambako chombo kinanelekea, au upande wowote anaoweza kuelekea kwa urahisi utakubaliwa.

## UDHU

Neno Udu linamaanisha kuosha sehemu fulani za mwili kwa kujitayarisha kusali. Hiyo ni sharti ya Sala ambayo haina budi kutimizwa; la sivyo Sala haitasihi. Mtume Muhammad s.a.w. alifundisha kuosha viganja vya mikono mara tatu wakati wa kutawadha. Kisha mtu asukutuwe maji kinywani mara tatu.




Tena atie maji puanī mara tatu na kuisafisha vizuri.




Kisha uso mzima uoshwe na maji mara tatu.



Kisha aoshe mikono yake mara tatu, kuanzia mkono wa kuume, hadi vikoni, viko navyo vioshwe.




Hapo uloeshe mikono na maji na upake kichwani mara moja, na pitisha kidole cha shahada cha mkono wa kuume katika sikio la kuume, na kile cha kushoto katika sikio la kushoto. Ncha za vidole hivyo zipitishwe vizuri kwa kusafisha mifuo yote ya masikio, na ziingizwe kiasi katika matundu ya masikio



Kisha viganja vipinduliwe, na sehemu za nyuma za viganja zipitishwe kutoka nyuma ya shingo kuelekea upande wa mbele ya shingo.



Mwishowe miguu ioshwe hadi mafundoni, mafundo yaki-oshwa pia, mara tatu kwa kuanzia mguu wa kuume. Kama kwa sababu fulani sehemu inaoshwa mara moja moja au mbili mbili, udhu utakamilika; hata hivyo njia bora ndiyo ile tunayokuta katika sunna ya Mtume Muhammad s.a.w., yaani kuosha sehemu zote mara tatu. Basi udhu umekwisha kamilika tayari.



Inapaswa ya kwamba baada ya kutawadha dua ifuatayo isomwe:

**اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي مِنَ التَّوَابِينَ وَاجْعَلْنِي مِنَ الْمُتَطَهِّرِينَ**

**Matamshi:** *Allahummaj'alni minat-tawwabina waj'alni minal-mutatahhirina.*

**Tafsiri:** E Allah, nijaalie niwe mionganoni mwa watubuo na nijaalie niwe mionganoni mwa waliotakasika.

Hii ndiyo njia ya kutawadha kikawaida ambapo mtu yu mzima, si mgonjwa na kiafya hakukatazwa kutawadha na maji. Pia ni sharti kwamba maji safi yapatikane. Kama mtu yu mgonjwa ama maji hayapo, hapo mtu anatakiwa kufanya Tayammum kwa njia ifuatayo:

Piga mikono yote miwili juu ya mahali penye vumbi safi. kama ukiona mikono yako imeshika vumbi jingi, pulizia mbali hiyo ziada. Kisha upake mikono yako usoni. Na baada ya kupaaka usoni upitishe kila kiganja kwenye sehemu za nyuma za mkono mwingine. Tayammum ndiyo mfano wa kutawadha kwa kukukumbusha kuwa ikiwezekana lazima utawadhe.

Mtu akisali, hana budi udhu wake uwe salama. Kama udhu wake haujatanguka, mtu anaweza kusali zaidi ya Sala moja kwa udhu huo huo mmoja. Hiyo yahakikisha ya kwamba lazima mtu awe na udhu pindi asalipo; siyo lazima atawadhe upya kwa kila Sala kama udhu wake haujatanguka.

## MAMBO YANAYOTANGUA UDHU

- a. Kutokwa na upepo (kushuta, kujamba).
- b. Kukojoa, hata kama tone moja tu la mkojo limetoka.
- c. Kwenda haja kubwa (kunya) hata kama umetokwa na kinyesi kidogo sana.

d. Kulala usingizi, kusinzia kiasi hiki kwamba kama hakuna kitu unachoegemea usingeweza kujizuia kuanguka.

e. Damu ya hedhi, na pia kutokwa na manii. hayo yamekwisha elezwa mapema.

f. Kuhusu kutapika na kutokwa na damu, maoni yanahiti-lafiana. Hata hivyo mtu akijikata kidogo na kisu na kadhalika damu kidogo sana ikitoka hiyo haitaharibu udhu. Kadhalika chakula kidogo kikitoka wakati wa kuteuka haitahesabika ni matapishi. Lakini mtu akitokwa na damu au akitapika hasa atatakiwa kutawadha upya.

Mtu akivaa soksi baada ya kutawadha, hapo halazimiki kuvua soksi na kuosha miguu wakati wa kutawadha tena. Bali anapaswa tu kulowesha mikono na maji na kupaka kila mguu juu ya soksi. Ruhusa hii inaendela hadi masaa 24 sharti asivue soksi. Msafiri anaruhusiwa kupaka juu ya soksi kwa muda wa siku tatu, usiku na mchana.

## **BAADHI YA HITILAFU ZA MUHIMU BAINA YA MAD- HEHEBU MBALIMBALI**

Sawa na fikhi ya Washia, miguu haioshwi katika udhu, bali kupaka maji miguu ndiyo sheria yao, bila kujali umevaa soksi ama hapana. Baadhi ya makundi yana maoni makali kama vile Mawahabii ambao wanasesma kwamba soksi hazipakwi maji hata kama ni za sufu ama pamba. Bali soksi hizo ziwe za ngozi nyembamba ambamo vumbi ama unyemvu haupenyi; soksi za aina hiyo zaitwa khuffi kwa Kiarabu. Hao wanasesma kupaka maji kunaruhusiwa juu ya khuffi siyo soksi.

Baadhi ya wengine ndio wakali zaidi na maoni yao ya kukazania mambo madogo huleta ugumu katika dini, jambo amabalo ni kinyume na moyo wa Islam. Mtume Mtukufu s.a.w. alisema:

## **إِنَّ الدِّينَ يُسْتَرٌ** (بخارى، كتاب الإيمان، باب الدين نسر)

Hakika Dini ni rahisi (Bukhari).

Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inaamini sana maneno hayo ya Mtume s.a.w. Waahamdiyya wanashika sera ya kutumia busara. Hivyo soksi kama ni nzito kiasi cha kutosha kuzuia uchafu, hapo swala kwamba soksi hizo zimetengenezwa kwa kitu gani halina maana yejote.

### **KUOGA MAJI**

Kuoga kunasisitizwa na kuhimizwa katika Islam. Islam haitilii mkazo usafi wa roho pekee bali na usafi wa mwili pia. katika baadhi ya hali fulani mtu amelazimishwa kuoga kabla ya kusali. katika hali zifuatazo mtu analazimika kuoga ambapo kutawadha peke yake hakutoshi:

#### **1. KWA MWANAMKE:**

- (a). Baada ya kutoka mwezini ambapo damu inakatika kabisa.
- (b). Baada ya kujifungua ambapo damu inakatika kabisa.

Kumbuka kwamba mwanamke hatakiwi kusali katika hali ya hedhi wala katika hali ya kupata damu ya uzazi.

#### **2. KWA WANAUUME NA WANAWAKE KWA JUMLA:**

- (a). Kutokwa na shahawa kwa sababu ya kuonana kimwili ama kwa sababu nyingine yoyote iwayo. Basi kutokwa na shahawa katika usingizi pia kutasababisha mtu aoge.
- (b). Kuonana hata kama shahawa haikutoka, na hata kama ni kwa kitambo kidogo tu.
- (c). Wasiokuwa Waislamu wanaposilimu wanapaswa kuoga na kuanza kuishi maisha mapya ya Kiislamu.

## **HALI NYINGINE AMBAZO KUOGA NI WAJIBU**

Mtoto azaliwapo anapaswa kuogeshwa. Kadhalika maiti anaoshwa kabla ya kuvishwa sanda na kusaliwa. Hata hivyo wale wanaokuwa shahidi katika njia ya Allah ama wanaouawa katika vita au wanaokufa kwa kushambuliwa hawana haja ya kuoshwa.

isitoshe, kuoga kila siku ya Ijumaa na siku za Idi mbili na kabla ya kuanza kuhiji kumesisitizwa sana na Mtume Mtukufu s.a.w.

Itapendeza kujua ya kwamba Mtume Mtukufu wa Islam s.a.w. alikuwa anaoga kwa njia ifuatayo:

Yeye alikuwa anatawadha kwanza na kisha akatia maji zile sehemu za mwili zilizo upande wa kuume mara tatu na kisha upande wa kushoto mara tatu na kisha akatia maji mwilini kwa jumla. Yeye alikuwa anaoga kwa uangalifu hata kwamba kinywele cha kila sehemu ya mwili wake kilisafishwa barabara.

Katika hali zote zile ambapo mtu analazimika kuoga, kusali hakusihi bila ya kuoga, na pia haruhusiwi kuingia msikitini wala kusoma Quran Tukufu. Lakini wanawake waliomo mwezini wanaweza kusoma Quran Tukufu lakini wasiiguse na mikono mitupu.

## **MAJI**

Maji yanayotumika kutawadha ama kuoga yanapaswa kuwa safi yasiyoathiri vibaya afya. Maji machafu hayapaswi kutumiwa. hata hivyo kama maji safi yasiyo na madhara yasipopatikana na watu kulazimika kutumia maji yoyote, basi na wayatumie kwa kutawadha vilevile na kuoga pia.

## **MAVAZI**

Katika Sala mtu anapaswa kujifunika mwili wake vizuri, hususan uchi wake na sehemu za pembeni mwake. Wanaume wanazimika kufunika angalau sehemu kutokea kitovu hadi magoti; magoti nayo yafunikwe. Lakini wanawake wanazimika kufunika mwili mzima isipokuwa viganja vyta mikono na miguu mpaka mafundoni. Naam, mwanamke akisali nyumbani au pamoja na wanawake wengine ambako hakuna wanaume wanaweza kuacha wazi nyuso zao.

## **KUFUNIKA KICHWA KWA WANAUUME**

Msimamo wa madhehebu mengi ni kwamba wanaume wanaplaswa kufunika vichwa vyao wakisali. Lakini Wa-malikii na baadhi ya wengineo hawaoni jambo hilo kuwa la lazima.

## **ADHANA**

Katika siku za mwanzoni ambapo Islam ilikuja kulikuwa hakuna njia maalum ya kuwajulisha watu kwamba saa ya Sala imewadia, wala haikuweko njia yoyote ya kuwaita Waislamu waje kusali Sala pamoja msikitini. Mtume Mtukufu s.a.w. alielewa ya kwamba Wayahudi, Wakristo na Mapagani wanazo njia kadha wa kadha za kuwaita watu kwenye ibada zao. Yeye alishauriana na Waislamu na kuwauliza tufanyeje kuwaita Waislamu msikitini kwa ajili ya kusali pamoja nyuma ya Imam.

Siku moja usubuhi Hadhrat Abdullah bin Azizi r.a. alimfikia Mtume Mtukufu s.a.w. na kumweleza njozi yake aliyoota usiku uliopita. Aliota kwamba mtu fulani anatangaza saa za Sala na kuwaita watu kwa sauti ya juu waje kusali msikitini pamoja. Kisha hadhrat Abdullah alisimulia yale maneno yenyewe ya adhana aliyopata kusikia katika njozi, nayo ndiyo yafuatayo:

***Allahu Akbar*** (mara nne)

Allah ni Mkuu kuliko kila kitu

اللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُ أَكْبَرُ

***Ashahadu alla ilaha Illallaah*** (mara mbili)

nashuhudia kwamba hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah.

أَشْهَدُ أَنَّ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ ، أَشْهَدُ أَنَّ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

***Ashhadu anna Mumamadr-Rasuulullaah*** (mara mbili)  
nashuhudia kwamba Muhammad ndiye Mjumbe wa Allah.

أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ ، أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ

***Hayya 'alas-Salaah*** (mara mbili)

حَيٌّ عَلَى الصَّلَاةِ ، حَيٌّ عَلَى الصَّلَاةِ

Njooni kusali.

***Hayya 'alal-Falaah*** (mara mbili)

Njooni kwenye ufaulu.

حَيٌّ عَلَى الْفَلَاحِ ، حَيٌّ عَلَى الْفَلَاحِ

***Allah Akbar*** (mara mbili)

Allah ni Mkuu kuliko kila kitu

اللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُ أَكْبَرُ

*Laa ilaala illallaah.*

Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah.

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

Hadhrat Umar r.a. ambaye akawa Khalifa wa Pili baadaye, pia alikuwa amekaa pamoja na Mtume s.a.w. wakati huo. Yeye alisema ya kuwa yeye naye alisikia maneno hayo hayo katika njozi yake. Hapo Mtume s.a.w. hakuwa na shaka kwamba huo ni ujumbe kutoka kwa Allah. Basi akakubali njia hiyo ya kutoa adhana ili kuwaita watu kusali msikitini. Hivyo, basi, adhana inatambulikana duniani kote kwa njia maalum ya Waislamu kuitana kwenye Sala.

### NJIA YA KUTOA ADHANA

Mwadhini, (mtoaji adhana) anapaswa kusimama mahali palipoinku ikiwezekana, akielekea kibla. Siku hizi kipaza sauti pia kinatumika kutoa adhana. Mwadhini anapaswa kugusa masikio yake kwa vidole vya shahada, sikio la kuume kwa kidole cha shahada cha mkono wa kuume na sikio la kushoto kwa kidole cha shahada cha mkono wa kushoto, na kutoa adhana kwa sauti ya juu. Anaposema 'Hayya Alas-Salaah' anapaswa kugeuza kidogo uso wake upande wa kuume; na wakati wa kusema Hayya Alal-Falaah ageuze kidogo uso wake upande wa kushoto.

Katika adhana ya Sala ya Alfajiri, mwadhini anatakiwa kusema baada ya 'Hayya Alal-Falaah' maneno yafuatayo mara mbili:

الصَّلَاةُ خَيْرٌ مِّنَ النُّومِ

*Assalaatu khairum-minan-Naum*

Sala ni bora kuliko usingizi.

Mtume s.a.w. alisema:

إِذَا سَمِعْتُمُ النَّدَاءَ فَقُولُوا مِثْلَ مَا يَقُولُ الْمُؤْمِنُونَ.

(حَارِي، بِخَاتَمِ الْأَذْانِ، بَابُ مَا يَقُولُ إِذَا سَمِعَ الْفَتَابِي)

**Matamshi:** *Idha sami'tumun-Nida'a faquluu mithla ma yaqulul Muadh-dhin.*

**Tafsiri:** Msikiapo adhan, semeni anayosema mwadhini.

Basi mtu anayesikia adhana ikitolewa anapaswa kurudia maneno ya adhana; lakini pindi mwadhini asemapo 'Hayya Alas-Salaah' na 'Hayya Alal-Falaah' hapo msikilizaji adhana aseme:

**Matamshi:** *Laa haula wala Qwwata illaa bilaahil-Aliyyil-Adhiim.*

**Tafsiri:** Hakuna uwezo wala nguvu isipokuwa kwa Allah.

Washia wanaongeza yafuatayo katika adhana yao:

أَشْهُدُ أَنَّ عَلِيًّا وَلِيُّ اللَّهِ

حَتَّىٰ عَلَىٰ خَبِيرِ الْعَمَلِ

**Matamshi:** *Ash-hadu anna Aliyyan waliyullaah Hayya Alaa Khairil-Amal.*

**Tafsiri:** Nashuhudia ya kwamba Ali ni Walii wa Allah. Njoo ni kwenye kitendo bora.

Baadhi ya madhehebu yanaongeza yafuatayo:

الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَيْكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ

**Matamshi:** *Assalaatu wassalaamu alaika ya Rasuulallaah.*

**Tafsiri:** Baraka na manai ziwe kwako, Ewe Mjumbe wa Allah.

Hatuelewi wanayo madaraka gani ya kuongeza hayo yote katika adhana. Tujuavyo sisi, maneno ya adhana tuliyoadhika

hapo juu ndiyo yaliyo sahihi. Hata kama Sala ya pamoja ina-saliwa uwanjani au nje ya msikiti, hata hivyo adhana yapaswa kutolewa kabla ya Sala. Adhana ikiisha tolewa, msikilizaji anapaswa kuomba hivi:

اللَّهُمَّ رَبَّ هَذِهِ الدَّرْعَةِ التَّامَّةِ وَالصَّلُوةِ  
الْقَائِمَةِ أَتِ مُحَمَّدًا لِوَسِيلَةٍ وَالْفَضِيلَةَ  
وَالدَّرِجَةَ الرَّفِيقَةَ وَابْنَ شَهَادَةِ مَقَامَ مُحَمَّدٍ  
إِلَّذِي وَعَذَّتْهُ إِنَّكَ لَا تُخْلِفُ الْوَيْمَارَدَ

**Matamshi:** *Alahumma Rabaa hadhi-hidda'watit-Taamaati wasswalaatil Qaaimati, Aati Muhammadanil Wasilata wal-fadhiilata, waddaraja-tarrafiaata, wab'ath-hu maqaamam-Mahmuudanilladhii wa'attahu. Innaka laa tukhliful mi'aad.*

**Tafsiri:** Ee Allah, Mola wa wito huu mkamilifu na Sala isimamayo, mfanye Muhammad kuwa njia (ya sisi) kukukurubia, na mpe daraja la juu na umnyanyue kwenye cheo kilichosifika ulichomwahidi. Hakika Wewe huvunji ahadi.

### KUKIMU SALA

Imam anapokwisha simama mahali pake ili kuongoza Sala, hapo Ikamah inatolewa. Ikamah ni adhana kwa kifupi. Kuna baadhi ya tofauti fulani baina ya maneno ya adhana na ya Ikamah ambazo ni hizi zifuatazo.

- i. Adhana inatolewa kwa sauti ya juu kabisa, lakini ikamah hutolewa kwa suati ndogo.
- ii. Wakati wa kutoa ikamah vidole vya shahada haviwekwi masikiioni kama inavyofanywa wakati wa kutoa adhana; bali mikono inanyoshwa tu ikining'inia kuelekea chini.
- iii. Maneno Assalaatu Khairum-Minan-Naum hayatamkwi

katika Ikamah.

iv. Maneno ya ikamah hutamkwa haraka haraka ambapo maneno ya adhana hutamkwa taratibu. Lakini Wamalikii wanatoa adhana na ikamah kwa sauti ya namna moja kwa kutulia sana baada ya kila fungu la maneno. Katika ikamah maneno haya yanaongezwa baada ya Hayya 'Alal-Falaah: Qad Qaamatis-Salaatu, Qad Qaamati-Salaah (maana yake: Sala imesimama; Sala imesimama).

v. Wakati wa kukimu (kutoa Ikamah) huelekei kuume na kushoto ukitamka Hayya 'Alas-Salaah na Hayya 'Alal-Falaah.

Maneno ya Ikamah huwa kama ifuatavyo:

اَللّٰهُ اَكْبَرُ اَللّٰهُ اَكْبَرُ اَشَهَدُ انَّ لَا إِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ  
اَشَهَدُ اَنَّ مُحَمَّداً رَسُولُ اللّٰهِ . حَسَنٌ عَلَى الْمَسْلُوَةِ  
حَسَنٌ عَلَى الْمُنْلَاجِ قَدْ قَامَتِ الْمَسْلُوَةُ  
قَدْ قَامَتِ الْمَسْلُوَةُ اَللّٰهُ اَكْبَرُ اَللّٰهُ اَكْبَرُ  
لَا إِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ -

**Matamshi:** *Allahu Akbar, Allahu Akbar. Ashahadu alla ilaha Illallaah. Ashhadu anna Mumamadr-Rasuulullaah. Hayya 'alas-Salaah. Hayya 'alal-Falaah. Qad Qaamati-Salaah, Qad Qaamati-Salaah. Allahu Akbar, Allahu Akbar. Laa ilaala illallaah.*

**Tafsiri:** Allah ni Mkuu kuliko kila kitu, Allah ni Mkuu kuliko kila kitu. Nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah. Nashuhudia ya kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allah. Njooni kwenye Sala, njooni kwenye ufaulu. Sala imesimama, Sala imesimama. Allah ni Mkuu kuliko kila kitu, Allah ni Mkuu kuliko kila kitu. Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah.

Mtume Mtukufu s.a.w. aliagiza ya kwamba mwadhini ndiyi

atakayetao Icamah (Tirmidh, Abwabus-Salaat, Babu Ma Ja'a Man adh-dhana fahuwa yakuuum). Namma, haja ikipatikana, mtu mwingine anaweza kukimu akiruhusiwa na mwadhini ama Imam.

## KUFUNGA NIA

Kufunga nia ni jambo la muhimu wakati wa kusali. Mwenye kusali afunge nia moyoni kwamba anasali Sala gani, ni ya faradhi ama sunna au nafali na kadhalika, na kwamba atasali rakaanngapi. Haimlazimu kutamka maneno maalum kwa sauti ya juu. Kufunga tu nia moyoni kunatosha. Mwenye kusali akifunga nia moyoni pia atamke Taujih - maneno ambayo tutayaandika mahali pengine katika mlango wa Pili.

## KUKUSANYA SALA

Katika baadhi ya hali fulani Sala mbili zinaweza kukusanya pamoja. Kwa mfano Sala ya Adhuhuri yaweza kukusanya pamoja na Sala ya Alasiri. kadhalika Sala ya Magharibi yaweza kukusanya pamoja na Sala ya Isha. Masharti ya kukusanya Sala mbili ni haya yafuatayo:

- a. Kama mtu yu mgonjwa.
- b. Kama mtu yuko safarini.
- c. Kama mvua inanyesha ama inapiga dhoruba.
- d. Kama ni vigumu kufika msikitini kwa sababu ya matope na kadhalika yaliyosababishwa na mvua kubwa.

Ni vizuri kukusanya Sala mbili katika wakati wa Sala hiyo ya kwanza. kwa mfano, ni afadhlali kukusanya Adhuhuri na Alasiri katika wakati wa Sala ya Adhuhuri. Hata hivyo kama kuna shida, waweza kukusanya Sala mbili wakati wa Sala hiyo ya pili. Pia ujue kwamba Adhuhuri na Alasiri zaweza kukusanya, na

kadhalika Magharibi na Isha zaweza kukusanya. Huwezi kkusanya Sala ya Alasiri na ile ya Magharibi ama Sala ya Isha na Sala ya Alfajiri.

Wakati wa kukusanya Sala mbili, adhana moja tu inatosha kwa Sala zote mbili, lakini ikamah itatolewa kwa kila Sala mbalimbali.

Pia ikumbukwe ya kuwa ukikusanya Sala mbili huna haja ya kusali sunna, bali Rakaa za Faradhi zinasaliwa. Naam, rakaa mbili za sunna haziachwi kabla ya Sala ya Ijumaa hata kama ukikusanya Sala ya Ijumaa na Sala ya Alasiri. Pia rakaa tatu za witri lazima zisaliwe hata ukikusanya Sala ya Magharibi na Isha.

Kama Sala mbili za Adhuhuri na Alasiri zinakusanya, na Imam baada ya kwisha kusalisha Adhuhuri amekwisha anza kusalisha Alasiri, hapo kama mtu anafika msikitini wala hajui kwamba Imam anasalisha Alasiri, mtu huyo aingie tu katika Sala nyuma ya Imam. Baadaye akijua kwamba Imam amesalisha Sala ya Alasiri, hapo yeye mtu huyo asali rakaa nne za Sala ya Adhuhuri, Sala ya Alasiri amekwisha sali nyuma ya Imam. Lakini aliyechelewa kufika msikitini akijua kwamba Imam anasalisha Sala ya Alasiri, mtu huyo asiungane na Imam, bali kwanza asali Sala yake ya Adhuhuri peke yake, ndipo akipata sehemu yoyote ya Alasiri nyuma ya Imam, asali naye. Kadhalika, kama Imam anaongoza Sala ya Isha, lakini mtu aliyechelewa kufika hajui, yeye anaweza kuungana na Imam akifikiria kwamba Imam anasalisha Sala ya Magharibi. Sala yake ya Isha itasihi, na baadaye asali peke yake rakaa tatu za Magharibi. Lakini akijua mapema kwamba Imam anaongoza Sala ya Isha, mtu huyo anapaswa kwanza asali Sala yake ya Magharibi peke yake ndipo aungane na Imam kusali ile sehemu iliyobakia ya Sala ya Isha. Kikawaida mtu anatakiwa kusali kwanza ile Sala ilio kwanza na kisha ile ya pili.

## **MLANGO WA PILI**

### **NJIA YA KUSALI**

Kikawaida Sala inapaswa kusaliwa pamoja msikitini, mahali palipotolewa kwa ibada ya Allah, lakini wakati mwengine kwa sababu fulani fulani mtu anaweza kusali mahali pengine pia sharti mahali hapo pawe safi.

Kabla mtu hajaanza kusali, ye ye anatakiwa awe safi wa mwili na awe na hakika ya kwamba nguo zake nazo ni safi. Kisha atawadhe na kusimama katika safu pamoja na waaminio wengine nyuma ya Imam, wote wakielekea Kaaba. Safu ni sharti ziwe zimenyooka, wasalio wote wakisimama bega kwa bega katika safu bila mmoja wapo kumtatiza mwenzake. Mtukufu Mtume s.a.w. alisisitiza mno kunyosha safu wakati wa kusali

Wakiisha simama katika safu nyuma ya Imam, maamuma wote wanuie kwamba wako tayari kusali Sala fulani, kisha watamke Taujih ifuatayo:

إِنِّي وَجَهْتُ وَجْهِي لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَاوَاتِ  
وَالْأَرْضَ حَتَّىٰ فَوْمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ

**Matamshi:** *Inni wajjahatu wajhiya lilladhii fataras-Samawaati wal-ardha hanifan wamaa ana minal-Mushrikiin.*

**Tafsiri:** Nimeelekeza uso wangu kwa Yule Aliyezungu mbingu na ardhi kwa kujihalisisha, nami simo mionganoni mwa washirikina.

Mara kabla ya Imam kuanza kusalisha, Ikama inatolewa ambayo ni namna ya kutangaza kwamba sasa Sala inasimamishwa.

Wakati wa kusali mtu anapaswa kutia moyo kikamilifu katika Sala na kujiepusha na mawazo mengine yote.


Sala inaanzia na kutamka Takbirah Tahrira. na njia ya kutamka Takbirah tahrira ni kwamba Imam anainua mikono yake hadi

kwenye ndewe za masikio yake na kutamka 'Allahu Akbar' (Al-lah ni Mkuu kuliko kila kitu), na maamuma wote wanafanya hivyo hivyo nyuma ya Imam.



Hiyo ni sunna ya Mtume s.a.w. Madhehebu yote ya Kiislamu yanaafikiana ya kwamba hiyo ni sunna. Lakini yapo baadhi ya madhehebu mengine ya Waislamu yanayoshika njia ya kuinua mikono yao zaidi ya mara moja katika rakaa moja. Wao wanainua mikono yao pia wanapoinama katika Rukuu, tena wakati wa kusimama wima baada ya rukuuu, tena wakati wa kwenda kusujudia na wanapoinuka kutoka kwenye sujuda. Tukiangalia historia, tunatambua ya kwamba Mtume s.a.w. alipata kuinua mikono yake zaidi ya mara moja katika Rakaa moja katika siku za mwanzoni kama tusomavyo katika vitabu vya Hadithi zake s.a.w., lakini hiyo haikuwa ni njia yake ya siku zote. Sawa na Hadithi nyngine nyngi, Mtume s.a.w. hakuinua mikono yake isipokuwa wakati wa kutamka Takbira Tahrima, yaani pindi aliapoanza kusali akatamka Alahu Akbar mwanzoni mwa Rakaa ya kwanza tu pekee. Sahaba mmoja wa Mtume s.a.w., Hadhrat Abdullah bin Mas'uud r.a. anasimuliwa ya kwamba safari moja akasema:

"Hebu niwaambie namna alivyokuwa akisali Mtume s.a.w. Kisha hadhrat Abdullah r.a. akasali na akainua mikono yake mara moja tu mwanzoni mwa Sala wakati wa kutamka Takbira Tahrima.



Baada ya kuinua mikono hadi ndewe za masikio na kutamka Allahu Akbar, Imam anateremsha chini mikono na kuifunga kifuani, mkono wa kuume ukiwa juu ya mkono wa kushoto. Hali hii ya mwenye kusali kusimama mbele ya Mola wake kwa unyenyekevu, akifunga mikono yake kifuani kwa adabu nydingi huitwa Qiyam. Naam, wako wengine wanaofunga mikono yao si kifuani bali kidogo chini ya kitovu, na wengine tena wanaofunga kidogo juu ya kitovu. Zote hizo shabaha yake ni kuonesha heshima na adabu, haifai kwa mtu kugombana juu ya mambo hayo madogo madogo ya hitilafu. Pia itambulikane ya kwamba Wamaliki (kutoka mionganoni mwa Wasunni) na Washia hawa-fungi asilani mikono katika Sala; wanainyosha ikielekea chini. Ijapokuwa haithibitiki kwamba Mtume s.a.w. aliwahi kufanya hivyo hata mara moja maishani, hata hivyo mtu hana haki ya kusema kwamba Sala ya watu hao wasiofunga mikono katika Sala haisihi. Baada ya kutamka Takbirat Tahrima, kila mmoja anatakiwa kusoma Thanaa; yaani kumtukuza Allah kwa maneno yafuatayo:

سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ فَتَبَارَكَ  
أَسْمَكَ وَتَعَالَى جَذْكَ وَلَا إِلَهَ غَيْرُكَ

**Matamshi:** *Sub-hana-kalla-humma wabi-hamdika, wa tabaara-kasamuka, wa ta'ala jadduka, walaa ilaaha ghairuka.*

**Tafsiri:** utukufu ni Wako, E Allah, na U pamoja na sifa zako njema. na jina lako ni lenye mibaraka. Na shani yako iko juu. Wala hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Wewe. (Tirmidhi, Kitabus-Salaah, Baabuz-Dhiki bainas-Salaati wa baina Qira'at). Imesimuliwa vilevile ya kwamba Mtume s.a.w. pengine alisoma maneno mengine ya kumtukuza Allah, lakini hayo hapo juu yanajulikana zaidi na kusomwa.

Baada ya Thanaa, inasomwa Ta'awwudh kimoyomoyo:

أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَنِ الرَّجِيمِ

**Matamshi:** *A'udhu billahi minash-shaitaanir-Rajiim.*

**Tafsiri:** Najikinga kwa Allah katika shari ya shetani mlaaniwa.

Kisha Imam anasoma Basmalah kimoyomoyo ama kwa sauti, lakini maamuma lazima wasome kimoyomoyo Basmalah yenewe ndiyo ifuatayo:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﷺ

**Matamshi:** *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim.*

**Tafsiri:** Kwa jina la Allah, mwangi wa Reheme, mwangi wa Ukarimu.

Sawa na hadithi, Mtume s.a.w. alisoma Tasmiyah kwa sauti na wakati mwagine kimoyomoyo. Baadhi ya Waislamu, kama vile katika nchi za Kiarabu, wanasoma tasmiyah kwa sauti lakini Wahafanifi na Waislamu wengine wengi wanasoma kimoyomoyo.

Kisha Imam anasoma sura Fatiha. katika Sala za Alfajiri,

Magharibi na Isha Imam anasoma sura Fatiha kwa sauti ya juu, lakini katika Sala za Adhuuhi na Alasiri anaisoma kimoyomoyo. Maamuma kwa vyovyote wanaisoma kimoyomoyo. Imam anapoisoma kwa sauti ya juu, maamuma wamfuate nyuma aya kwa aya kimoyomoyo katika nafasi baina ya kila aya mbili. Sura Fatiha ndiyo hii:

الْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِينَ □ الرَّحْمٰنُ الرَّحِيْمُ □  
مَلِكُ يَوْمٍ الدُّنْيَا □ إِلٰا كَ تَعْبُدُ وَ إِلٰا كَ تَسْعَيُونَ □  
إِهْدِنَا الْقِرَاطَ الْمُنْتَقِيمَ □ جَرَأْتَ الْبَيْنَ أَتَعْمَلُ عَلَيْهِمْ □  
غَيْرُ الْمَغْضُوبُ عَلَيْهِمْ وَلَا الْمَأْتَىْنَ □

**Mtamshi:** *Alhamdu Lillahi Rabbil 'Alamiin. Ar-Rahmaanir-Rahiim. Maaliki yaumid-Diin. Iyyaka na'budu wa iyyaka nast'a'iin. Ihdinas-Swiraatal mustaqiim. Swiratalla-dhiina an'amta 'alaihim. Ghairil magh-dhuubi 'alaihim waladh-dhaalliin.*

**Tafsiri:** Sifa zote njema zinamhusu Allah, Mola wa walim-wengu. mwingi wa rehema, mwingi wa ukarimu, Mmiliki wa siku ya malipo. Wewe tu twakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada. Tuongoze njia iliyonyooka, njia ya wale Uliowaneeme-sha, si ya wale Uliowakasirikia, wala ya wale waliopotea.

Wakisha maliza sura fatiha, maamuma wasema 'Amin', maana yake, Ee Allah, tupokelee dua yetu.

Wamalikii, Washafii na Wahambalii hutamka Amin kwa sauti kubwa, lakini Wahafafii hutamka kimoyomoyo. Njia zote mbili ni sawa. Hilo si mionganoni mwa mambo ambayo unayategemea usahihi ama uharibifu wa Sala. Mtu aweza kushika njia yoyote anayopenda. Akipenda aseme kwa sauti kubwa na akitaka aseme kimoyomoyo. Mtu mwiningine asimwingilie kati; isipokuwa mtu akitamka kwa sauti ya juu kabisa na kuchafua Sala ya wengine. Kishapo Imam asome sehemu yoyote ya Quran Tukufu, sura ndogo ama kwa uchache aya tatu. Kwa mfano:

## SURA ALKAUTHAR

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ۝ إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ  
فَصُلِّ لِرَبِّكَ وَانْحَرْ ۝ إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْرَرُ ۝

**Matamshi:** *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim. Inaa a'tainaakal Kauthar. Fasalli lirabbka wanhar. Inna shaaniaka huwal abtar.*

**Tafsiri:** Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, mwingi wa ukarimu. Hakika Tumekupa heri nyingi. Basi usali kwa Mola wako na utoe dhabihu. Hakika adui wako atakuwa mkiwa

## SURA ALIKHLAS

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ۝ قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ۝ اللَّهُ الصَّمَدُ  
لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُوْلَدْ ۝ وَلَمْ يَكُنْ لَّهَ كُفُوءٌ أَحَدٌ ۝

**Matamshi:** *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim. Qul huwallahu ahad. Alla-husswamad. Lam yalid. Walam yuulad. Walam yakullahuu kufuhan ahad.*

**Tafsiri:** Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, mwingi wa ukarimu. Sema: Yeye Allah ni Mmoja, Allah Asiyehitaji, Ambaye wote wanahitaji Kwake. Hakuzaa wala Hakuzaliwa. Wala hakuna afananaye naye hata mmoja.

## SURA ALFALAQ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ۝ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ۝  
مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ ۝ وَمَنْ شَرِّ عَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ۝  
وَمَنْ شَرِّ الظَّفَرِ فِي الْعُقَدِ ۝ وَمَنْ شَرِّ حَارِسِ إِذَا حَسَكَ ۝

**Matamshi:** *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim. Qul a'udhu birabbil falaq. Min sharri maa khalaq, wamin sharri ghaasiqin*

*idha waqab, wa min sharrin Naffathaati fil 'uqad, wamin sharri hasidin idhaa hasad.*

**Tafsiri:** Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, mwinci wa ukarimu. Sema najikinga kwa Mola wa mapambazuko, (Anilinde) katika shari ya Alivyoviumba, na katika shari ya giza la usiku liingiapo, na katika shari ya wale wanaopuliza mafundoni, na katika shari ya hasidi anapohusudu.

### SURA ANNAS

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ۖ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ۖ  
رَبِّ الْأَنْوَارِ ۖ إِلَوَالنَّارِ ۖ مِنْ شَرِّ أَوْسُورِيْمَهُ الْخَاتِمِ ۖ  
الَّذِي يُوَسُّعُ فِي صَدْرِ النَّاسِ ۖ مِنْ أَكْبَارِهِ وَالْأَقْرَبِ ۖ

**Matamshi:** *Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim. Qul a'udhu birabbin-Naas, malikin-Naas, Ilaahin-Naas; min sharril waswaasil khannaas. Alladhi yuwawisuu fii suduurin-Naas. Minal jinnati wan-Naas.*

**Tafsiri:** Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, mwinci wa ukarimu. Sema: ninajikinga kwa Mola wa watu, Mfalme wa watu, Mwabudiwa wa watu, katika shari ya wasiwasi (wa shetani) aendaye kisirisi kwa hila, atiaye wasiwasi miyoni mwa watu, miongoni mwa majinni na watu.

Sura hizo chache tulizoandika juu ni mifano tu. Imam anaweza kuchagua sehemu yoyote ya Quran kwa kusoma baada ya Sura Fatiha.

Pindi Imam asomapo sehemu ya Quran Tukufu, maamuma wanapaswa kusikiliza wakiwa kimya, maana Quran inaagiza:

وَإِذَا قُرِئَ الْقُرْآنُ لَا سَمِعُوا لَهُ وَالصُّمُّ أَعْلَمُ بِمَا يُحِنُّونَ


**Tafsiri:** na Quran inaposomwa, basi isikilizeni na nyamazeni ili mpate kurehemewa. (7:205).

Sahaba mmoja wa Mtume s.a.w., Hadhrat Ubada bin Samit r.a., anasimulia ya kuwa safari moja Mtume s.a.w. alipokuwa akiongoza Sala ya Alfajiri aliona shida kusoma aya za Quran kwa sababu ya minong'ono nyuma yake. Mtume s.a.w.alipomaliza Sala yake akawauliza masahaba zake kwamba walikuwa wanasona aya za Quran kumfuata yeye usomaji wake? Wakajibu, Naam: Hapo Mtume s.a.w. akasema:

Msisome aya za Quran nyuma ya Imam isipokuwa Sura Fatiha, kwani Sura Fatiha ndiyo sehemu hasa ya Sala isiyoweza kutenganishwa.

Ni jambo la muhimu kabisa ya kwamba mtu ye yeyote asifanye lolote la kuvuruga Sala ya wenzake. kwa hiyo, kila Mwislamu anapaswa kuzingatia hadithi hiyo ya Mtume s.a.w. hapo juu.

Akiisha kusoma sehemu ya Quran, Imam anainama kwenda katika hali ya Rukuu akitamka Takbira (Allahu Akbar). Maa-muma wote wanamfuata kwenda katika Rukuu. Ndani ya Rukuu, mkono wa kuume ulibonyeze goti la kuume, na mkono wa kushoto goti la kushoto, na sehemu ya juu ya mwili kutokea kiuno hadi kichwa huwekwa katika mstari mtambaa.



Katika Rukuu, kila moja anapaswa kusoma Tasbihi ifuatayo kimoyomoyo mara tatu ama zaidi kwa idadi ya witri:

## سُبْحَانَ رَبِّيَ الْعَظِيمُ

**Matamshi:** *Subhaana Rabbiyal Adhiim.*

**Tafsiri:** Utukufu ni wa Mola wangu, mwenye adhama.

Kisha Imam anasimama wima akinyosha mikono yake ikining'inia chini ubavuni. Anapaoanza kusimama wima anatamka Tasmii kwa sauti ya juu kuwajulisha maamuma kwamba ye ye amesimama wima sasa baada ya Rukuu.

Tasmii ndiyo ifuatayo:

## سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمَدَهُ

**Matamshi:** *Sami'allahu liman hamidah.*

**Tafsiri:** Allah kamsikiliza aliyemsifu.

Hapo maamuma wote wanamwitikia Imam na kusema Tahmiid ifuatatyö:

## رَبَّنَا لَكَ الْحَمْدُ ، حَمْدًا كَثِيرًا طَبِيتاً مُبَارَكًا فِيهِ

**Matamshi:** *Rabbanaa wal-akal hamdu. Hamdan kathiran tayyiban mubaarakan fihi.*


**Tafsiri:** Mola wetu, ni zako sifa zote njema zilizo nyingi ambamo mna baraka.

Kusimama wima baada ya Rukuu huitwa Qauma inayoiishia kwa kusema Tahmiid.

Hapo tena Imam anatamka Takbira na kuanguka katika



sujuda. Yeye kwanza anaweka magoti yake chini, tena kichwa pia. Katika hali hii, magoti, mikono, pua na paji la uso vyapaswa kugusa chini. Paji la uso liwe chini baina ya mikono miwili; Mikono kutokea viwiko hadi vikoni isiguse chini asilani na itenganishwe na ubavu.



Mtume s.a.w. alisema kuhusu sujuda: Mnapomsujudia Allah, mnapaswa kuweka chini mikono yenu na miguu yenu kwa njia iliyosawa. Kwa vyovyote msitandaze chini mikono yenu jinsi atandazavyo mbwa wakati wa kukaa. (Masnad Ahmad bin Hambal, J 3, Uk. 279, Maktaba Islami, Beirut).

Katika hali ya sujuda, vidole vyá mikono vielekee kibla. Miguu iwe chini ilhali vidole vyá miguu vielekee kibla.

Katika hali ya sujuda, Tasbih ifuatayo inasomwa kwa uchache mara tatu kimoyomoyo. Kama anataka kusoma mara zaidi ya tatu asome mara ambayo ni witri, yaani idadi isiyogawanyika sawasawa na mbili:

## سُبْحَانَ رَبِّيِ الْأَعْلَىٰ

**Matamshi:** *Subhaana Rabbiyal A'laa.*

**Tafsiri:** Utukufu ni wa Mola wangu Aliye juu.

Sujuda ni hali ya unyenyekevu mkubwa kabisa, kujitupa na unyonge sana ambako mwenye kusali anatoa moyo wake mbele ya Allah Mwenye nguvu na kumwomba msamaha.

Izingatiwe ya kuwa Mtume s.a.w. alikataza kusoma aya za Quran katika hali ya Rukuu na Sajdah (Muslim, Kitabus-Salaah, Bab Annahyi 'an Qira'atil Quran Fir-Rukuu was-Sujuud).

Kisha Imam anatamka Takbira tena ambapo Imam pamwe na maamuma wote wanainua kwanza kisha mikono kutoka chini na wanaketi hali inayoitwa Jilsa. Katika Jilsa, mwenye kusali analaza mguu wake wa kushoto na kuketi juu yake ilhali mguu wa kuume umesimama lakini vidole vyake vinaelekea kibla. Viganja vya mikono vinawekwa juu ya mapaja na vidole vinaelekea kibla. katika hali hii dua ifuatayo inasomwa:

رَبِّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَاهْدِنِي وَعَافِنِي

وَاجْبِرْنِي وَارْزُقْنِي وَارْفَعْنِي

**Matamshi:** *Allahumma magn-firlii, warhamnii, wahdinii, wa 'afinii, warfa'ni, wajburnii, warzuqnii.*

**Tafsiri:** E Allah, nisamehe na nirehemu na niongoze na nilinde na balaa na ila na nin-yanyue na niungie na niruzuku.



Baada ya Jilsa, Imam anawaongoza maamuma kusujudia mara ya pili kwa kutamka Takbira. Hapo tena "Subhaana Rabbiyal A'laa" husemwa mara tatu au zaidi kwa idadi iliyo witori. katika kila Rakaa huwa sujda mbili kila mara. Ukiisha maliza sujuda ya pili, Rakaa yako moja imekamilika. Sasa Imam anatamka Takbira tena na kuwaongoza maamuma kwenye hali ya kusimama wima ili kuanza kusali Rakaa ya pili kama ilivyosaliwa Rakaa ya kwanza. Lakini katika Rakaa ya pili, Thanaa na ta'awwudh hazisomwi. Thanaa na ta'awwudh husomwa katika Rakaa ya kwanza peke yake. Katika Rakaa ya Pili, Imam anasoma Sura fatiha na aya chache za Quran Tukufu na anamaliza Rakaa ya pili hadi sujuda ya pili. Baada ya sujuda ya pili hasimami alivyosimama katika Rakaa ya kwanza, bali sasa anaketi jinsi alivyoketi katika Jilsa. Kuketi huku mwishoni mwa Rakaa ya pili huitwa Qaidah.


Katika hali hiyo inasomwa Tashah-hud ifuatayo:

السُّجُودُ لِلَّهِ وَالصَّلَاةُ وَالطَّبَابُ ، ، السَّلَامُ  
 عَلَيْكَ أَنْهَا إِلَيْكَ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ . السَّلَامُ عَلَيْكَ  
 وَعَلَىٰ عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ ، اتَّهَدْ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ  
 وَأَنَّهُدْ أَنْ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ

**Matamshi:** *Attahiyyatu lillahi waswalawatu wattayyibatu. Assalaamu alaika ayuhan-Nabiyyu warahmatullahi wa barakaatuh. Assalaamu 'alaikum wa 'ala 'ibadillaahis-Swalihiin. Ashhadu allaa ilaaha illallaahu wa ash-hadu anna Muham-madan abduhuu wa Rasuuluh.*

**Tafsiri:** Maamkizi yote ya heshima na unyenyekevu ni kwa Allah na pia Sala zote na vyote vilivyohalisika. Salamu iwe kwako, Ewe Nabii, na rehema za Allah na baraka zake. Salamu iwe kwetu sisi na kwa watumishi wema wa Allah. Nashuhudia ya kuwa hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah. Na ninashuhudia

ya kuwa Muhammad ni mtumishi wake na Mtume wake.



Izingatiwe ya kwamba asaliye asomapo Tashah-hud akifikia maneno 'Ash-hadu alla ilaaha illallaahu' anapaswa kunyosha juu kidole chake cha shahada cha mkono wa kuume na kukirudisha pindi amalizapo hayo. Imesimuliwa katika vitabu vya Hadithi za Mtume s.a.w. ya kwamba Mtume Mtukufu s.a.w. alipokuwa anaketi katika Tashah-hud alikuwa akiweka mkono wake wa kuume juu ya goti lake akikunja vidole vyake vitatu kwa kuacha kidole cha shahada na kidole gumba, na kukinyosha juu kidole cha shahada wakati aliposoma maneno Ash-hadu allaa ilaaha illallaah, na kisha kuteremsha hicho kidole baada ya kumaliza hayo maneno na kukirudisha katika hali ya kwanza. Vidole vya mkono wa kushoto vinanyooshwa juu ya goti la kushoto.

Baada ya kwisha kusoma tashah-hud, inasomwa Sala ya Mtume s.a.w., pamoja na baadhi ya dua nyingine kimoyomoyo.

### SALA YA MTUME S.A.W.

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَّ عَلَى الْمُخْمَدِ كَمَا  
صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَّ عَلَى أَلِّ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مُّجِيدٌ  
اللَّهُمَّ بارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَّ عَلَى الْمُخْمَدِ كَمَا  
بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَّ عَلَى أَلِّ إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مُّجِيدٌ

**Matamshi:** *Allahumma swalli 'alaa Muhamadin wa 'alaa aali Muhamadin kamaa swallaita 'alaa Ibraahiima wa 'alaa aali Ibraahiima, Innaka hamiidum-Majiid. Allahumma baarik 'alaa Muhamadin wa 'alaa aali Muhamadin kamaa baarakta 'alaa Ibraahiima wa 'alaa aali Ibraahiima, Innaka hamiidum-Majiid.*

**Tafsiri:** E Allah, msalie Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama ulivyomsalia Ibrahimu na wafuasi wa Ibrahimu. Hakika Wewe ndiwe Uhimidiwaye Utukukaye. E Allah, mbariki Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama Ulivyombariki Ibrahimu na wafuasi wa Ibrahimu. Hakika Wewe ndiwe Uhimidiwaye Utukukaye.

Sala ya Mtume s.a.w. inafuatwa na ombi fupi ama maombi ambayo baadhi yake ndiyo yafuatayo:

رَبَّنَا آتَنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَّ فِي الْآخِرَةِ حَسَنَةٌ وَّ قَاتَلَنَا دَارَ

**Matamshi:** *Rabbanaa aatinaa fidduniya hasanatan wafil Aakhirati hasanatan. Waqinaa adhaaban-Naar.*

**Tafsiri:** E Mola wetu, Tujaalie wema katika dunia na wema katika akhera. Na tulinde na adhabu ya Moto.

رَبِّنَا أَجْعَلَنَا مُقِيمَ الْمَضْلُوَةِ وَمِنْ ذُرَيْتِنَا رَبَّنَا وَتَقْبَلَ دُعَاءُنَا

رَبَّنَا اغْفِرْنَا وَلَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ وَلَكُلُّ مُنْزَنْ يَوْمَ يَقُولُ الْحِسَابُ

**Matamshi:** *Raabij-'alnii muqimas-Swalati wamin dhurriyyatii . Rabbanaa wa taqabal du'a. Rabbanagh-fir li wa liwalidayya walil-muminina yauma yaquumul hisaab. (Sura Ibrahimu: 41:42).*

**Tafsiri:** E Mola wetu, nijaalie niwe mwenye kusimamisha Sala na pia wazao wangu. Ee Mola wetu, na nipokelee dua yangu. Mola wetu, nisamehe mimi na wazazi wangu na waaminio siku ya kusimama hesabu.

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْهُمَّةِ وَالْحُزْنِ ، وَأَعُوذُ بِكَ  
مِنَ الْفَجْرِ وَالْكُسْلِ ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الدُّجَى وَالْبَخْلِ ،  
وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ غَلَبةِ الظَّفَرِ وَقُبْرِ الرِّجَالِ

**Matamshi:** *Allahumma innii a'udhu bika minal-hammi wal-huzni. Wa a'udhu bika minal-'ajzi wal-kasli. Wa a'udhu bikaminal-jubni wal-bukhli. Wa a'udhu bika min ghalabatid-daini wa qahrir-rijaali.* (Abu Dawud, Kitabus-Swalaah, Babulisti -'dhah).

**Tafsiri:** E Allah, najikinga kwako dhidi ya matatizo na huzuni. Na ninajikinga kwako dhidi ya unyonge na uzembe. Na ninajikinga kwako dhidi ya woga na ubahili. Na ninajikinga kwako dhidi ya kuelemewa na deni na ukorofi wa watu.

اللَّهُمَّ إِنِّي ظُلِمْتُ نَفْسِي طَلْمًا كَبِيرًا ، وَلَا يَغْفِرُ اللَّهُ تَوْبَةً  
إِلَّا أَنْتَ لَأَغْفِرْلَى مَغْفِرَةً مِنْ عِنْدِكَ ، وَلَا حَمْنَى  
إِنْكَ أَنْتَ الْغَفُورُ الرَّجِيمُ


**Matamshi:** *Allahumma, innii dhalamtu nafsi dhulman kathiiran, walaa yaghfirudh-dhunuuba illa anta. Faghfiri lii maghfiratam-min in-dika warhamnii. Innaka antal-gha-fuurur-Rahiim.*

**Tafsiri:** E Allah, nimejidhulumu nafsi yangu sana. Wala hakuna awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Wewe, basi nig-hofirie dhambi na nirehemu. Hakika Wewe ndiwe Msamehev u Mwingi wa ukarimu.

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ ، وَأَعُوذُ بِكَ  
مِنْ فِتْنَةِ الْمُسِيحِ الدُّجَى ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا  
وَفِتْنَةِ الْمَمَاتِ ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ النَّارِ وَالنَّعَمَ

**Matamshi:** *Allahumma, inni a'udhu bika mina adhabil qabri, wa a'udhu bika min fitnatil-masihid-dajjaali, wa a'udhu bika min fitnatil mahya wal-mamaati. Allahumma, inni a'udhu bika minalma'thami wal-maghrami.*

**Tafsiri:** Ee Allah, najikinga kwako dhidi ya adhabu ya kaburi, na ninajikinga kwako dhidi ya fitina ya masihi-dallaji, na ninajikinga kwako dhidi ya fitina ya uhai na fitina ya mauti. E Allah, ninajikinga kwako dhidi ya kufanya dhambi na dhidi ya kuwa na deni. Baada ya kusoma dua mojawapo ama zaidi katika hiso hapo Imam anatoa salamu, yaani anageuza uso wake upande wa kuume na kusema Assalaamu alaikum wa Rahmatullah, maana yake salamu iwe kwenu na rehema ya Allah. Kisha anageuza uso wake upande wa kushoto na kusema pia Assalaamu 'alaikum wa Rahmatullaah. Imam anatoa salamu kuonesha kwamba anamaliza Sala. Na ndivyo wanavyofanya maamuma wote pia. Kama Sala inayosalisha si ya Rakaa mbili bali ni ya Rakaa tatu au nne, hapo muda wa kuketi katika Qa'adah mwisho wa Rakaa ya pili, unafupishwa na mwenye kusali atasoma hadi mwisho wa Tashahhud. Baada ya Tashahhud Imamu anasema Allahu Akbar na kusimama Qiyam kumaliza Rakaa zilizosalia kama vile alivyosalisha Rakaa ya kwanza na ya pili; huku maamuma wote wakimfuata.



Kama Sala yenye inayosalisha ni ya Rakaa tatu, kama Sala ya Magharibi, hapo Imam baada ya sujuda ya pili ya Rakaa ya Tatoo anaketi katika hali ya Qa'dah na anasoma Tashahhud, Sala ya Mtume s.a.w. na baadhi ya dua kimoyomoyo na anatoa Salamu kumaliza Sala yake. Maamuma wote nao wanamfuata katika mambo hayo yote.

Na kama Sala ni ya rakaa nne kama vile Sala ya Adhuhuri, Alasiri na Isha, hapo Imam hakai katika Qa'dah baada ya rakaa ya Tatoo, bali akiisha fanya sujuda ya pili anasimama wima katika hali ya Qiyam akitamka Takbir ili kuanza Rakaa ya nne. Maamuma wote nao wanamfuata na kusimama wima. Rakaa ya nne inasaliwa kama Rakaa ya pili na baada ya sujuda ya pili Imam anaketi katika hali ya Qa'dah inayoitwa Qa'dah ya mwisho. Hapo anasoma Tashahhud, Sala ya Mtume s.a.w., baadhi ya dua na anatoa salamu kulia na kushoto kama ilivyokwisha elezwa hapo juu.

Mambo yafuatayo yanafaa yazingatiwe:

- i. Kama ni Qa'dah ya mwisho, hapo baada ya Tashahhud pia usome Sala ya Mtume s.a.w. na dua nyinginezo. kama siyo Qa'dah ya mwisho, utasoma Tashahhud pekee na utainuka ukisema Allahu Akbar na kuanza Rakaa nyingine.
- ii. Kama ni Sala yenye Rakaa mbili, Qaidah baada ya Rakaa ya pili ndiyo Qa'dah ya mwisho.
- iii. Kama Sala ni ya Rakaa tatu, Qa'dah baada ya Rakaa ya tatu ndiyo Qa'dah ya mwisho.
- iv. Kama Sala ina Rakaa nne, Qa'dah baada ya rakaa ya nne ndiyo Qa'dah ya mwisho.

## SALA YA MTU PEKE YAKE

Hata kama mtu anasali peke yake, si nyuma ya Imam, atasali kabisa jinsi anavyosali akiwa nyuma ya Imam, isipokuwa yale maneno anayosoma Imam kwa sauti ya juu (ili kuwasikilizisha maamuma) mtu hyo hatasoma kwa sauti ya juu, bali atayasoma kimoyomoyo. kwa mfano, asomapo Sura Fatiha ama atamkapo Takbir, au asemapo Sami'allahu liman Hamidah na atoapo salam, yeye atasema kimoyomoyo.

## SALA YA PAMOJA NA JAMAA

Kila Mwislamu (mwanamume) anatakiwa asali sehemu ya Sala ilio Fardh (Faradhi) pamoja na jamaa. Misikiti hujengwa kwa ajili ya Sala kusaliwa pamoja na jamaa nyuma ya Imam. Imeelezwa katika hadithi moja ya kwamba thawabu ya Sala inayosaliza pamoja na Imam ni mara ishirini na saba zaidi kuliko Sala anayosaliza mtu peke yake.

Imam anafaa achaguliwe na maamuma na awe mtu ambaye sawa na ujuzi wa maamuma ndiye mcha Mungu na mjuzi wa Quran Tukufu. Imam pia anaweza kuwekwa na mkuu wa utaratibu wa dini kama upo, kama vile Khalifa. mtu yejote anayechaguliwa ama kuwekwa kuwa Imam hana budi afuatwe katika Sala hata kama maamuma yejote akidhani kwamba Imam aliyewekwa hafai kuwa Imam. Kwa wale wanaotilia shaka ustahilivu wa Imam, agizo lifuatalo la Mtume s.a.w. liwatosheleze:

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: الْمَسْلُوَةُ الْمَكْتُوَبَةُ وَاجِبَةٌ خَلْفُ كُلِّ مُسْلِمٍ، بَأْرَأْ كَانَ أَوْ فَاجِرًا فَإِنْ عَمِلَ الْكَبَائِرَ۔ (سنن أبي ذاود، الجزء الأول، كتاب المسلاة)

**Matamshi:** '*An Abi Huraira Qaala, qaala Rasulullahi s.a.w. Assalaatul-Maktuubatu wajibatun khalfa kulli Musalimn, Baarran kana au faajiran, wa in 'amilal kaabaair (Sunan Abi Dawud, Kitabus-Salaah).*

**Tafsiri:** Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira ya kwamba Mjumbe wa Allah alisema: Ni wajibu kusali Sala ya faradhi nyuma ya kila Mwislamu akiwa mwema au mbaya na hata kama ametenda dhambi kubwa.

Kama wakati wa Sala yoyote wanaume wawili au zaidi wanakuwa pamoja mbali na msikiti, basi wanatakiwa kusali Sala hiyo pamoja. Kama wanaume wawili tu wakisali pamoja, mmoja wao atakuwa Imam. Hao wawili watasimama safu moja, maamuma akiwa upande wa kuume wa Imamu.

Pengine mtu anasali nyumbani, na mionganini mwa watu wa nyumbani mmojawapo aliye wa kike anataka kusali pamoja naye, hapo huyo wa kike atasimama upande wa kushoto wa Imam. Kama Waislamu wawili wanaume wanasali pamoja na kisha wanafika maamuma wengine, hao maamuma wanapaswa kuipanga katika safu kwa namna ambayo Imam atakuwa katikati. Kikawaida Waislamu watatu ama zaidi wakisali pamoja, Imam husimama mbele yao peke yake, wote wakielekea kibla. Lakini kama kuna haja, Imam anaweza kusimama katikati ya maamuma katika safu ya kwanza.

Sawa na madhehebu fulani wakati wa kusali Sala pamoja haina budi watu kwa uchache wawili wapatikane katika safu ya mwisho nyuma ya Imam. Wenye imani hiyo wanamruhusu aliyechelewa kufika msikitini kumrudisha taratibu mmojawapo wa safu ya mwisho nyuma ili kufanya safu mpya kwa watu wawili badala ya mtu huyo mpya kusimama peke yake katika safu. Lakini kuna madhehebu ambayo hayapendi hivyo, kwani kitendo hicho si tu kinatatiza Sala ya yule anayeletwa nyuma

bali kinatatiza pia Sala ya wengine wa safu hiyo ambao wamo katika ibada.

## **MAMBO MENGINEYO YA KUZINGATIWA**

1. Maamuma wa safu ya kwanza wanapata thawabu zaidi kuliko maamuma wa safu ya pili sawa na hadithi moja ya Mtume s.a.w. Kwani wale wanaofika mapema wanaendelea kumkumbuka Allah wakingojea Sala. Hivyo hao wako katika ibada muda wote huo kuliko wale wanaofika baadaye. Tena Mtume s.a.w. aliagiza kwamba safu mpya isianzishwe isipokuwa kwanza safu ya mbele ikamilike. Hivyo, ni dhahiri shahiri ya kwamba anaotangulia kufika na kukaa katika safu ya kwanza na kutumia mrefu zaidi katika kumkumbuka Allah, watapata thawabu nyingi kuliko wanaofika saa za mwisho ambapo takbirat Tahrif inatamkwa au hata kwa kuchelewa zaidi. Hao ndio wanaosimama katika safu za nyuma.

2. Kama mtu amechelewa kufika katika Sala, yeye mtu huyo ataungana na wengine moja kwa moja katika ile sehemu ya Sala waliyomo maamuma wengine. Kwa mfano, kama wako katika hali ya kusimama wima (qiyam), mwenye kuja kwa kuchelewa ataungana nao katika hali hiyo ya Qiyam. na kama wako katika hali ya sujuda, basi huyo naye ataingia katika hali ya sujuda pamoja nao.

Imam amalizapo Sala kwa kutoa salamu kwa kusema Assalaamu alaikum wa Rahmatullah kulia na pia kushoto, hao yule aliyechelewa atasimama wima (Qiyam) bila kutoa salam ili kulipa Rakaa hiyo ama hizo ambazo hakuweza kusali pamoja na Imam.

3. Sala ina mafungu. Kila fungu huitwa Rakaa, Sala ya faradhi inaweza kuwa ya Rakaa mbili au tatu au nne.

Kila Rakaa inazo sehemu zifuatazo zilizo za muhimu:

i. Hali ya kusimama wima iitwayo Qiyam

ii. hali ya kuinama kwa kuweka mikono juu ya magoti iitwayo Rukuu.

iii. Hali ya kusimama wima baada ya kuinama iitwayo Qauma.

iv. Hali ya kusujudia iitwayo Sajdah.

v. Jilsa: Hali ya kuketi baina ya sujuda mbili.

vi. Qa'dah; hali ya kukaa baada ua sujuda zote mbili.

Kama mwenye kuchelewa anaungana na wengine kabla au ndani ya hali ya kuinama (Rukuu), huyo atahesabiwa kwamba amekwisha pata Rakaa hiyo nzima; hana haja tena kuilipa baada ya Imam kumaliza Sala. Na kama alichelewa zaidi na hakupata kuungana na wengine katika hali ya Qiyam ama Rukuu bali kaingia katika sehemu iliyo baada ya Rukuu, hapo yeye atatakiwa kuilipa Rakaa hiyo baada ya Imam kumaliza Sala akiisha toa salamu kulia na kushoto.

4. Sala ya jamaa nyuma ya Imam ikiisha anza tayari, mtu asianze kusali Sala ya sunna ama nafali. Kama alikuwa amenza kusali sunna kabla ya Imam hajaanza kusalisha, anapaswa kuvunja Sala yake hiyo ya sunna na kuungana na maamuma wengine mara moja kama anajikuta yuko katikati ya safu ya maamuma. Na kama yuko mbali na safu ya maamuma, hapo akiona kwamba hatakosa Rakaa ya kwanza nyuma ya Imam anaweza kuendelea na sunna ama nafali zake na kuzimaliza. La sivyo, anatakiwa kuvunja Sala yake hiyo na kuungana na wengine nyuma ya Imam.

5. Kama Sala imekwisha anza kusaliwa na Imam, mtu amekatazwa kukimbia na kuungana na jamaa nyuma ya Imam. Bali atembee kikawaida na kufika na kuingia nyuma ya Imam katika sehemu yoyote anamomkuta Imam.

6. Kwa kuwastahi na kuwaheshimu, wanawake hawasi-mamishwi mbele ya wanaume katika Sala. kwa hiyo safu za kina mama siku zote huwa nyuma ya safu za wanaume. kwa njia hiyo wanawake wanapata uhuru wa kusali katika safu za nyuma bila kutatizwa na kuwepo wanaume. Hata hivyo ni

afadhali kwamba kina mama wawekewe sehemu maalum msikitini kwa kuweka pazia baina ya sehemu ya wanaume na sehemu ya wanawake. Pia ni dhahiri kutokana na ilivyosemwa hapo juu kwamba mwanamke hawezi kuwasalisha wanaume, lakini anaweza kuwasalisha kinamama wengine. Ndiyo kusema kwamba mwanamke anaweza kuwasalisha wanawake pamoja na watoto, wa kike na wa kiume, lakini si wanaume waliobalehe.

7. Wanawake hawana haja ya kutoa adhana. Mama anayeon-goza (Imam) asimame katikati ya safu ya kwanza pamoja na maamuma wanawake wala si mbele yao kama anavyosimama Imam mwanamume mbele ya maamuma.

8. Kama Imam akikosea katika Sala, njia ifuatayo inatumika ili kumfahamisha kuhusu kosa alilofanya:

i. Kama kosa lenyewe linahusu usomaji wa Quran, au kama Imam amesahau aya fulani, hapo maamuma yeyote anayekumbuka vizuri maneno hayo anapaswa kumkumbusha Imam kwa kusoma hayo maneno taratibu kwa sauti inayoelewaka.

ii. Kama Imam anafanya kosa jingine, maamuma yeyote anapaswa kumwelekeza kwa kusema Subhanallah. Subhanallah maana yake ni kwamba Allah ndiye asiyefanya makosa. Hiyo itamwashiria Imam kwamba amekosea. Na ili kurekebisha kosa lake Imam atafanya sujuda mbili kabla ya kutoa salamu kuli na kushoto mwishoni mwa Sala, na maamuma wote pia watamfuata katika hizo sujuda mbili. Na kama Imam harekebishi kosa lake, maamuma bado wanatakiwa kuendela na kumfuata Imam wala hawana ruhusa ya kuhitilafiana naye. naam, baada ya kwisha kumaliza Sala Imam anaweza kuambiwa kuhusu kosa lake, na hapo Imam awaongoze maamuma kusujudi sujuda mbili ny- ingine kwa kurekebisha kosa alilolifanya katika Sala. Sujuda hizo mbili zaitwa Sajdatas-Sahwi, yaani sujuda mbili za kusahau.

9. Kama mwanamke anataka kumweleza Imam kwenye kosa lake, yeye asiseme Subhanallah, bali apige makofi. Sauti ya makofi itamkumbusha Imam kwamba amefanya kosa.

Na kama Imam wa kike anafanya kosa katika Sala, wanawake maamuma wanaweza kumkumbusha kwa kusema Subhanallah ama kwa kusoma maneno yale ya aya aliyoyakosea Imam sawa na hali ilivyo.

10. Imam asirefushe sana Sala hata kuwachosha maamuma. Azingatie kwamba nyuma yake kuna wengine walio wazee ama wagonjwa na pia wale wanaotakiwa kwenda kazini haraka baada ya kusali.

### **KUMKUMBUKA ALLAH BAADA YA KUMALIZA SALA**

Kuendelea kumkumbuka Allah kwa muda kidogo baada ya kumaliza Sala kwa kusoma Tasbih na Tahmid ndiyo agizo la Quran Tukufu. Allah anasema katika sura ya 4, aya ya 104:

**فَإِذَا قَضَيْتُمُ الصَّلَاةَ فَادْكُرُوا اللَّهَ**

Mkimaliza Sala basi mkumbukeni Allah.

Hiyo imethibitika kutoka sunna ya Mtume s.a.w. pia. Imesimu liwa na Hadhrat Aisha r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alikuwa anaendela kukaa baada ya kumaliza Sala na kusoma yafuatayo:

**اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلَامُ وَمَنْكَ السَّلَامُ ، بِأَنْتَ مَحْكُومُونَ فِي الْعَدْلِ وَالْأَكْرَامُ**

**Matamshi: Allahumma antassalaamu wa minkassalaamu tabarakta ya dhal jalaali walikraam.**

**Tafsiri:** E Allah u amani, Na amani ya kweli hutoka kwako. Una mibaraka ewe Mwenye Utukufu na ukarimu. (*Sahih Muslim, Kitabul Masaajid wa Mawadhi'us-Salaah, Baab Istihbadh-Dhikri Ba'das-salaah*).

Pia imesimulia katika vitabu vya hadithi ya kwamba wakati mwingine Mtume s.a.w. akakaa pamoja na masahaba zake na kui-nua mikono kwa kuwaombea wale waliomwomba waombewe. Hata hivyo, iliyo dhahiri kutoka katika hadithi iliyosimuliwa na hadhrat Aisha r.a. hapo juu ni kwamba haikuwa kawaida ya siku zote ya Mtume s.a.w. kuinua mikono baada ya Sala kwa kuomba kimoyomoyo. Habari hii ya Mtume s.a.w. kuomba baada ya Sala mara moja moja imechukuliwa kwa kukosea kuwa desturi ya siku zote. Matokeo ni kwamba baadhi ya madhehebu ya Kiislamu yanaichukua kuwa sunna ya Mtume s.a.w. ya siku zote, ilhali hiyo haikuwa kawaida yake ya kila siku kama iliyovoelezwa katika hadithi hapo juu. Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inaamini kuinua mikono baada ya Sala haikuwa kawaida ya Mtume s.a.w. Bali desturi yake siku zote ilikuwa ni kuketi kwa muda baada ya kusali na kumkumbuka Allah pasipo kuinua mikono.

Zaidi ya dua iliyotajwa hapo juu, dua hizi zifuatazo pia alizisoma Mtume s.a.w. baada ya Sala.

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ  
وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَوِيرٌ ، اَللَّهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا اغْتَسَلْتَ  
نَفْسِي بِهِ لِمَا نَفَعَتْ وَلَا يَنْقُضُ ذَا الْجَمِيعِ مِنْكَ الْجَمِيعُ

**Matamshi:** *La ilaaha illallaahu wahdahuu la shariika lahuu.  
Lahul mulku, wa lahul hamdu. Wa huwa alaa kulli shain qadiir.*

*Allahumma laa maani'a limaa a'taita, walaa mu'tiya limaa mana'ta, walaa yanfa'u dhal-jaddi minkal-jaddu (Sahih Bukhari, Kitab-Swalaah, Baab Adh-dhikr baadas-Swalaah).*

**Tafsiri:** Hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hakuna mshirika wake. Ufalme ni wake na sifa zote njema ni zake, naye ndiye Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

Ee Allah, hakuna awezaye kuzuia kile Utoacho Wewe. Wala hakuna atoaye kile Ukizuiacho. Wala shani haiwezi kumnufaisha mwenye shani dhidi yako.

اللَّهُمَّ إِعْنَى عَلَى ذِكْرِكَ وَشُكْرِكَ وَخَسِنْ عِبَادَتِكَ

**Matamshi:** *Allahumma a'inii alaa dhikrika wa shukrika wa husnii ibaadatika.*

**Tafsiri:** Ee Allah, nisaidie niweze kukumbuka na kukushukuru na kukuabudu sana.

سُبْحَانَ رَبِّ الْعَزَّةِ عَمَّا يَصْفُونَ وَسَلَامٌ  
عَلَى الْمُرْسَلِينَ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

**Matamshi:** *Subhaana Rabbika Rabbil Izzati 'aama yas-wifuun. Wasalaamun 'alal-Mursaliin. Walihamdu lillaahi Rabbil 'Alamiin.*

**Tafsiri:** Ameepukana Mola wako, Mola mwenye enzi, na yale wanayomsifu. Na amani iwe juu ya Mitume. Na sifa zote njema zamhusu Allah, Mola wa walimwengu.

Kwa kuombwa na baadhi ya masahaba, Mtume s.a.w. ali-waambia maneno yafuatayo kwa kumtukuzza Allah. Baadhi ya watu wameyachukua kama ni kawaida ya siku zote. Izingatiwe ya kwamba hilo si agizo hasa kikawaida. Basi siyo jambo la lazima sana kuyasoma mara baada ya Sala msikitini.

- a. Subhanallah, Utukufu ni wa Allah: yasomwa mara 33.
- b. Alhamdu Lillahi, Sifa zote njema zamhusu Allah. Yasomwa mara 33.
- c. Allahu Akbar. Mungu ni Mkuu kuliko vyote: yasomwa mara 34.

### **AINA ZA SALA NA RAKAA ZAKE.**

Ziko aina nne za Sala:

- 1. Fardh.    2. Waajib.    3.      Sunnah.          4.      Nafl

### **SALA ZILIZO FARDH**

Fardh maana yake ni Faradhi, yaani Sala zilizo za lazima kabisa.  
Ziko Sala tano za faradhi zifuatazo:

<b>SALA</b>	<b>IDADI YA RAKAA</b>
Fajr	2
Dhuhr	4
Asr	4
Maghrib	3
Isha	4

Ni dhambi kabisa kuacha Sala ya faradhi kusudi. Lakini kama mtu alisahau ama hakuweza kusali kwa sababu zisizoepukika, hapo kosa hilo lirekebishwe kwa kusali Sala hiyo mara baada ya kukumbuka ama haraka iwezekanavyo.

### **SALA ZILIZO WAJIBU**

Sala zifuatazo ndizo Sala zilizo Waajibu, yaani zile amabazo Mwislamu anawajibika kuzisali:

- 1. Rakaa tatu za Witri

2. Rakaa mbili za Sala ya idil-Fitri, na Rakaa mbili za Sala ua idil Adh-ha

3. Rakaa mbili zinazosaliwa wakati wa kuizunguka Kaaba (tawaaf).

Kama mtu anaziacha hizo kusudi, ye ye anafanya dhambi. lakini akisahau hizo halazimiki kuzikidhi. Qadhaa ndiyo kukidhi, yaani kutekeleza wajibu baada ya kupita muda wake hasa.

## SALA ZILIZO SUNNA

Mtume wa Islam s.a.w. alikuwa anasali Rakaa zaidi ya Rakaa za Faradhi. Rakaa hizo zinaitwa Sala za Sunna. Sawa na maoni wa wataalmu wote wa fikihi, Mwislamu hana budi kuzisali Sala za Sunna. mtu akiziacha kusudi anafanya kitendo cha kulaumiwa na Allah. Sala za Sunna ni hizi zifuatazo:

1. Rakaa mbili kabla ya Sala ya faradhi ya Alfajiri. lakini mtu akichelewa kufika msikitini na akakuta Imam amekwisha anza kusalisha Sala ya Alfajiri, hapo mtu anatakiwa aungane na Imam kwanza, kisha baada ya kumaliza Sala nyuma ya Imam asali rakaa mbili za Sunna.

2. Rakaa nne kabla ya Sala ya Adhuhuri. Na asipoweza kuzisali kabla ya Adhuhuri, hapo azisali baada ya kumaliza Sala ya Adhuhuri nyuma ya Imam.

Zingatia: Waislamu wa Ahmadiyya ambao mara nyingi wanaliifua dhehebu la Wahafafii husali Rakaa nne za sunna kabla ya Sala ya Adhuhuri na Rakaa mbili baada ya Sala ya Adhuhuri. Pia wapo Waislamu wengine wanaosali Rakaa nne za sunna kabla ya Sala ya faradhi ya Adhuhuri na Rakaa nne tena baada ya Sala ya Adhuhuri.

.3 Rakaa mbili za baada ya Sala ya Magharibi.

4. Rakaa mbili za sunna baada ya rakaa nne za Faradhi ya Isha.

## **SALA ZA NAFALI**

Waislamu wanasali, zaidi ya Sala za Faradhi na sunna, Sala za hiari vilevile. Sala hizo za hiari zinaitwa Sala za Nawafil ama Sala za Nafali. Wanaosali Sala za nafali wanufaika mno kiroho na wanamkurubia Allah sana.

Sala za nafali ndizo zifuatazo:

1. Rakaa nane za Sala ya Tahajjud.
2. Rakaa mbili baada ya kwisha maliza Sala nzima ya Ad-huhuri
3. Rakaa nne kabla ya Sala ya Alasiri.
4. Rakaa mbili baada ya kumaliza sunna mbili za Sala ya Magharibi.
5. Rakaa nne za Sala ya ishraaq.
6. Rakaa mbili mara baada ya kuingia msikitini.
7. Rakaa mbili wakati wa kumwomba Allah baraka zake.
8. Rakaa mbili za Salaatil Hajah.
9. Rakaa mbili za kumtolea Allah shukurani.

Ziko Sala nyingine za nafali ambazo zitatajwa mbele kitabuni humu.

Mtu anaweza kusali Sala nyingi zaidi anavyopenda za nafali, lakini Sala hizo za nafali zisisaliwe katika nyakati zilizokatazwa. Kwa mfano Sala ya nafali isisaliwe baada ya kusali Sala ya Alasiri hadi jua kutwa. Pia ni afadhali kuzisali Sala za nafali humo nyumbani kuliko msikitini, isipokuwa zile Sala za nafali zilizolezwa kwamba zinasaliwa msikitini. Hata hivyo hiyo ndiyo hiari ya mtu wala hakuna cha kumlazimisha.

## **SALA YA IJUMAA**

Salatul-Jumu'ah, Sala ya Ijumaa, husaliwa pamoja nyuma ya Imam. Sala hiyo insaliwa badala ya Sala ya Adhuhuri. Kila wiki siku ya Ijumaa Waislamu wanapaswa kuoga, kuvaa nguo nzuri

sana walizo nazo, kutumia manukato na kuhudhuria msikitini kwa ajili ya Sala ya Ijumaa. Quran Tukufu na Sunnah zinaelezea baraka nyingi sana za Sala ya Ijumaa. Kama Mwislamu anapitisha siku ya Ijumaa akimkumbuka Allah na kumwomba Yeye, Mwislamu huyo anajaaliwa thawabu nyingi sana.

Katika Sala ya Ijumaa Waislamu wa mji au kijiji kizima wanakusanyika pamoja. Katika miji mikubwa Sala ya Ijumaa inaweza kusaliwa mahala zaidi ya pamoja ili Waislamu wasipate matatizo. Kusanyiko hilo linawapa nafasi ya kuonana na kujadiliana matatizo yao ya kijamii na ya kibinafsi na kuyatatulia mbali. Kukusanyika pamoja mara moja katika juma kunaleta Umoja, kusaidiana na muungano baina ya Waislamu. Sala ya Ijumaa pia ni alama ya kuonesha usawa wa Kiislamu.

Siku ya Ijumaa Imam anapata nafasi ya kuwaongoza kuhusu mambo ya muhimu yanayowakabili. Hotuba ya Imam inawapa mwongozo sawa na mafunzo ya Kiislamu. Sala ya Ijumaa ni ya faradhi kwa kila Mwislamu mwanamume aliyebalehe. Lakini wagonjwa, vipofu, ama waliolemaa, wasafiri na wanawake hawakulazimishwa kuhudhuria Sala ya Ijumaa msikitini. Hao wanaweza kufika kusali Sala ya Ijumaa wakipenda, lakini wasiposali Sala ya Ijumaa watasali Sala ya Adhuhuri badala yake, kwani Sala ya Ijumaa husaliwa badala ya Sala ya Adhuhuri.

Ziko adhana mbili kwa Sala ya Ijumaa. Adhana ya kwanza hutolewa wakati jua linapopinduka kuteremka, na adhana ya pili inatolewa wakati Imam anaposimama kutoa hotuba. Adhana ikiisha tolewa, Imam anaanza kuwahutubia watu.

Hotuba ya Ijumaa ina sehemu mbili. Katika sehemu ya kwanza Imam baada ya kusoma Ta'awwudh na Sura Fatiha anawatolea mawaihda kwamba waaminio watekeleze maamrisho ya Allah na kutimiza wajibu wao ili kuwa Waislamu safi. katika hotuba jambo lolote jingine la muhimu laweza kuzungumzwa. Sehemu hiyo ya hotuba inaweza kutolewa katika lugha yoyote iwayo.

Baada ya kumaliza sehemu ya kwanza ya hotuba, Imam anaketi kwa kitambo kidogo kisha anainuka tena na kutoa

sehemu ya pili ya hotuba ambayo ndiyo kwa lugha ya Kiarabu, nayo ndiyo hii ifuatayo:

الْحَمْدُ لِلّٰهِ رَحْمٰنُو رَحِيمٌ وَسَبَّابِيْنَ وَسَبَّابِرَةَ  
وَتَوْمَنِ بِهِ وَتَوْكِلُ عَلَيْهِ . وَتَعُوذُ بِاللّٰهِ مِنْ شُرُورِ الْفَسَادِ وَ  
مِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا ، مَنْ يَهْدِي اللّٰهَ فَلَا مُضِلٌّ لَهُ وَمَنْ يَضْلِلُ  
فَلَا هَادِيٌ لَهُ . وَتَشْهِدُ أَنَّ لَّا إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ وَحْدَهُ  
لَا شَرِيكَ لَهُ وَتَشْهِدُ أَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ  
عِبْدُ اللّٰهِ رَجُلُكُمُ اللّٰهُ إِنَّ اللّٰهَ يَأْمُرُ بِالْمُعْدُنِ وَالْإِخْتَانِ  
وَإِيَّاهُ ذِي الْقُرْبَى وَرَيْهُ عنِ الْمُحْكَمَ وَالْمُنْكَرِ وَالْمُبَيْنِ  
يَعْظِمُكُمْ لَعْلَكُمْ تَذَكَّرُونَ اذْكُرُوا اللّٰهَ يَدْكُرُكُمْ وَإِذْغُرُوهُ  
يَسْتَحْجِبُ لَكُمْ وَلَدِكُمُ اللّٰهُ أَكْبَرُ

**Matamshi:** *Alhamdu Lillaahi, nahmaduhuu wa nastaa'iinuhuu, wa nastaghfiruhuu, wa nu'minu bihi, wa natawakkalu 'alaihi. Wa na'uudhu billaahi min shuruuri anfusinaa, wa mni sayyi'aati a'maalinaa. Man yahdihillahu falaa mudhillalahu, wa man yadhlilhu falaa haadiya lahu. Wa nash-hadu al-laah ilaha illallaahu wahdahuu la sharika lahuu, wa nash-hadu anna Muhammadaan 'abduhuu wa Rasuuluh. Ibaadallaahi, rahimakumullaah. Innallaaha ya'muru bil-'adli wal-ihsaani wa iitai dhil-qurbaa. Wa yanhaa 'anil fahshaai walmunkari walbaghyi. Ya'idhukum la'alakum tadhakkaruun. Udhkurullaaha yadhkurkum, wad'uhu yastajiblakum. Wa ladhikrullaahi Akbar.*

**Tafsiri:** Sifa zote njema zinamhusu Allah. Twamhimidia na twamwomba msaada; na twamwamini na twamtegemea. Na twajikinga kwa Allah dhidi ya shari za nafsi zetu na matendo yetu mabaya. Yule ambaye Allah anamwongoza, hakuna wa kumpoteza. Na yule ambaye Yeye anamhukumu kwamba

amepotea, hakuna wa kumwongoza. Na twashuhudia kwamba hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah akiwa peke yake asiye na mshirika. Na twashuhudia kwamba Muhammad ndiye mtumishi wake na Mtume wake. Enyi watumishi wa Allah, Awarehemuni Allah. Hakika Allah Anaamuru kufanya uadilifu na hisani na kuwapa wengine jinsi wanavyopewa jamaa wa karibu. Na Anawakatazeni maovu yanayohusiana na mtu binafsi, na maovu yanayowaathiri wengine na kuwaasi wenye madaraka. Anawatoleeni mawaidha ili mzingatie. Mkumbukeni Allah, Naye Atawakumbukeni. na mwombeni Atawapokeleeni. Na kumkumbuka Allah ndio wema mkuu.

Waisalmu wanatakiwa kusikiliza hotuba kwa makini. Ma-ongezi ya aina yoyote yamekatazwa wakati hotuba inapotolewa. Imam akiisha toa sehemu ya pili ya hotuba ndipo ikama inatolewa na hapo Imam anasalisha Rakaa mbili za Sala ya Ijumaa.

Mtume Mtukufu wa Islam s.a.w. hakutoa kibali hata kwa mtu kuwasihii wengine kunyamza pindi Imam aendeleapo kutoa hotuba. Kama kuna haja sana, mtu anaweza kumwashiria kwa mkono ama kidole yule anayezungumza wakati hotuba inapotolewa kwamba anyamaze. kama Imam anamwuliza mtu jambo fulani wakati wa kutoa hotuba, hapo mtu huyo anapaswa kumjibu.

Ni afadhali mtu aliyetao hotuba aongoze Sala pia. Imam asome Sura Fatiha na aya nyingine kadha za Quran Tukufu kwa sauti kubwa katika Sala ya Ijumaa. Mtu anatakiwa asali Rakaa nne za sunnah kabla ya Sala ya pamoja nyuma ya Imam, na pia Rakaa nne za sunna baada ya Sala ya Ijumaa ya Faradhi; lakini inaruhusiwa kusali Rakaa mbili badala ya Rakaa nne baada ya Rakaa mbili za faradhi za Sala ya Ijumaa kam ilivyoelezwa katika kitabu mashuhuri cha Hadithi kitiwacho Sunan Abi Dawud (Kitabus-Salaah, Baab Assalatu ba'dal Jumu'ah wa sharah As-Sunnah J3, uk. 449). Mtu akiwa safarini pia anawajibika kusali sunnah kabla ya Sala ya ijumlaha, lakini Rakaa mbili tu.

Mtu akichelewa kufika msikitini ambapo hotuba inaendelea kutolewa, yeye mtu huyo asijaribu kupita mbele kwa kuruka safu za watu wengine waliokaa mapema. Kwa kuwa hotuba imekwisha anza tayari, hivyo akipenda aweza kusali Rakaa mbili za sunna haraka haraka. Kama mtu amechelewa sana na akafika msikitini ilhali Imam yuko katika Qa'dah ya mwisho, mtu huyo aungane na Imam katika Qa'dah; lakini Imam akiisha toa salam kulia na kushoto, mtu huyo asimame bila kutoa salam na asali Sala nzima, Rakaa zote mbili, kwani yeye hakuwahi hata Rakaa moja pamoja na Imam. Na kama akifika ilhali Imam amekwisha maliza Sala nzima, yaani amekwisha toa salam, hapo mtu huyo atasali Sala yake ya Adhuhuri, Rakaa nne, badala ya Sala ya Ijumaa.

## **SIKU KUU ZA IDIL FITRI NA IDIL ADH-HA**

Ziko sikukuu mbili za Idi katika mwaka. Moja inaitwa Idil Fitri na ya pili inayofuata wiki 10 baadaye inaitwa Idil Adh-ha.

Idil Ftri inasherehekewa unapomalizika mwezi wa kufunga. Siku hiyo Waislamu wanafurahia kujaaliwa uwezo wa kutimiza wajibu wa kufunga saumu.

Idil Adh-ha inasherehekewa tarehe 10 mwezi wa Dhul-Hijjah kwa kukumbuka utii wa Hadhrat Ibrahimu a.s. na mwanawе Hadhrat Ismail a.s. Allah akakubali kujitolea kwao na utifu wao na kuwaelekeza kuchinja mwanakondoo kama dhabihu badala ya hadhrat Ismail a.s. Waislamu wanaokusanyika Makkah kwa kuhiji, wanachinja dhabihu zao siku hiyo ya Idi kubwa wakimfuata Nabii Ibrahimu mfano wake. Kitendo hiki cha kutoa dhabihu ya wanyama hurudiwa na Waislamu wa dunia nzima.

Waislamu wote, wanaume kwa wanawake na watoto pia, wanakusanyika pamoja siku ya idil Fitri na Idil Adh-ha ili kusali Rakaa mbili katika uwanja wa wazi nje ya kijiji ama mji, ikiwezekana.

Siku ya Idi, asubuhi na mapema, Waisalmu wakubwa kwa wadogo wanaoga na kuvala mavazi mazuri waliyo nayo. Watoto hususan wanavaa nguo mpya. Wote wanaume kwa wanawake wanatumia manukato pia kwani hiyo ilikuwa ni sunna ya Mtume s.a.w. kutumia uturi siku kama hiyo. Waislamu wanapika vyakula vizuri katika siku za Idi.

Siku ya Idil Fitri, mtu anapaswa kutoa fitri kabla hajasali Sala ya Idi. Pesa za fitri hutolewa kwa wenyewe hali ndogo ili nao waweze kushiriki katika sherehe za Idi. kila mmoja katika familia anapaswa kutoa fitri sawa na kima kinachokadiriwa kila mwaka sawa na hali. Fitri hutolewa kwa niaba ya watoto wachanga pia, na wazazi wanapswa kutoa fitri hata kwa niaba ya mtoto aliyezaliwa kabla ya Sala ya Idi.

Mtu anapaswa kupata kifungua kinywa barabara kabla hajaenda kusali Sala ya Idil-Fitri. Lakini kuhusu Idil Adh-ha imesimuliwa ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alipendelea kutokula kabla hajachinja mnyama wake wa dhabihu. Nyama ya dhabihu hiyo ikawa chakula chake cha kwanza siku hiyo; lakini hata hivyo kula mapema kabla ya hapo hakukatazwi.

Sawa na sunna ya Mtume s.a.w., Waisalmu wanakwenda kwenye uwanja wa kusali Idi kwa njia moja na kurejea makwao kwa njia nyininge.

Wakati wa Sala ya Idi unaendelea hadi saa sita ambapo jua linakurubia kufika kichwani. Kama vile Sala ya Ijumaa, Sala ya Idi pia husaliwa pamoja nyuma ya Imam. Lakini hakuna adhana wala ikama kwa Sala ya Idi.

Katika rakaa ya kwanza ya Sala ya Idi, baada ya kwisha kutamka Takbirah Tahlim na kusoma Thanaa lakini kabla ya kusoma Ta'awwudh, Imam ananyanya mikono yake hadi ndewe za masikio mara saba akitamka Allahu Akbar kila mara kwa sauti kubwa na kuteremshwa mikono kila mara. Na akiisha tamka Takbirah ya saba anafunga mikono kikawaida na anaendela na Sala. Maamuma nao wanainua mikono kila mara hadi ndewe za masikio na kutamka Takbirah, lakini si kwa sauti kubwa bali

kimoyomoyo na kushusha mikono kila mara ikining'inia chini. Katika Rakaa ya pili ziko Takbira tano zinazotamkwa kabla ya kusoma Sura Fatiha. Imam na maamuma wote wanainua mikono mara tano hadi ndewe za masikio na kuteremsha mikono kila mara ikining'inia ubavuni, lakini mara ya tano baada ya kutamka Takbira mikono inafungwa kama kawaida.

Mwisho wa Rakaa ya pili, baada ya kusoma Tashah-hud, Sala ya Mtume na baadhi ya maombi kadhaa, Imam anaelekeza uso wake kuume akisema Assalamu alaikum wa Rahmatullaah, kisha upande wa kushoto pia akitoa salamu hivyo hivyo ili kuonesha kwamba amemaliza Sala.

Baada ya kuongoza Sala ya Idi, Imam anatoa hotuba. Hotuba ya Idi inazo sehemu mbili kama vile hotuba ya sala ya Ijumaa. Izingatiwe ya kwamba hotuba ya Ijumaa inaitangulia Sala ya Ijumaa, lakini hotuba ya Idi inatolewa baada ya kwisha kusali Sala ya Idi.

Baada ya kumaliza kusali Sala ya Idil adh-ha, Imam na maamuma wote wanatamka maneno yafuatayo ya kumtukuzza Allah kwa sauti inayosikika:

اللهُ أَكْبَرُ، اللهُ أَكْبَرُ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ  
وَاللهُ أَكْبَرُ، اللهُ أَكْبَرُ، وَلِلَّهِ الْحَمْدُ

**Matamshi:** *Allahu Akbar, Allahu Akbar; Laa ilaaha illal-laahu, wallahu Akbar. Allahu Akbar, wa lillaahil-ahamdu.*

**Tafsiri:** Allah ni Mkuu kuliko vyote; Allah ni Mkuu kuliko vyote. Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah. Na Allah ni Mkuu kuliko vyote, Allah ni Mkuu kuliko vyote, na sifa zote njema zamhusu Allah.

Kadhalika hayo maneno hapo juu hutamkwa baada ya kila Sala ya faradhi kutokea tarehe 9 ya Dhul-Hijjah tangu Sala ya Alfajiri hadi Sala ya Alasiri tarehe 13 Dhul-Hijja.

**Kumbuka:** Kuyatamka maneno hayo hapo juu wakati wa kwenda uwanjani kusali Sala ya Idi na pia wakati wa kurudi nyumbani baada ya ibada ya Idi ndiyo sunna ya Mtume s.a.w.

## SALA YA WITRI

Witri maana yake ni idadi isiyoweza kugawanyika sawasawa mara mbili. Sala ya Witri inazo rakaa tatu nayo husaliwa baada ya kwisha kusali Sala ya Isha. Inapendekezwa kusoma Sura A'laa, Sura Kafiruun na Sura Ikhlaas katika Rakaa tatu za witri. lakini hata hivyo siyo lazima kusoma sura hizo tu, waweza kusoma sura zozote ama aya zozote za Quran Tukufu. Katika Rakaa ya tatu baada ya Rukuu mtu akisimama wima anapaswa kusoma Ombi la Kunuuut lifuatalo:

اللَّهُمَّ إِنَّا نَسْأَلُكَ وَنَسْتَغْفِرُكَ وَنَوْكِلُ عَلَيْكَ  
وَنَتَبَّعُ عَلَيْكَ الْخَيْرَ وَنَشْكُرُكَ وَلَا تَنْكِحْنَاكَ وَنَخْلُعُ  
وَنَتَرْكُ مَنْ يَقْبَرُنَا هُنَّمُ اللَّهُمَّ إِيَّاكَ نَعْلَمُ وَلَكَ نُسْأَلُ  
وَنَسْأَدُ وَإِلَيْكَ نَسْعَى وَنَجْدُ وَنَرْجُوا  
رَحْمَتَكَ وَنَخْشِي عَذَابَكَ ، إِنَّ عَذَابَكَ بِالْكُفَّارِ شَدِيدٌ ه

**Matamshi:** *Alahumma inaa nasta'inuka, wa nastaghfiruka, wa nu'minu bika, wa natawakkalu 'alaika, wa nuthnii 'alaikal khaira. Wa nashkuruka walaa nakfuruka, wa nakh-la'u wa natruku man yaffjuruk. Allahumma, iyyaaka na'budu, wa laka nuswallii wa nasjudu, wa ilika nas'a wa nahfidhu, wa narjuu Rahmataka, wa nakhshaa 'adhaabaka. Inna 'adhaabaka bil-Kuffaari mulhik.*

**Tafsiri:** Ae Allah, twakuomba msaada na twakuomba msa-maha. Na twakuamini na twakutegemea, na twakutolea sifa

njema. Na twakushukuru wala sisi sio wasiokuwa na shukurani kwako. Na twatengana na anayekuasi na twaachana naye. Ee Allah, Wewe tu twakuabudu na twasali kwa ajili yako na twakusujudia Wewe, na twakukimbilia na twaharakia. Na twatumai kupata rehema yako na twaiogopa adhabu yako. Hakika adhabu yako itawashika makafiri.

## **SEHEMU MBALIMBALI ZA SALA**

Sehemu mbalimbali za Sala zimepangwa katika vifungu kadha sawa na umuhimu wa hizo sehemu katika Sala.

## **FARDH - SEHEMU ZILIZO FARADHI**

Sehemu zilizo za lazima sana mno hata kwamba bila hizo Sala haisihi zinaitwa Fardh, yaani faradhi, za lazima.

Kama mtu ataacha sehemu ya faradhi, Sala yake haitasihi. Lakini mtu akiacha kwa kuisahau sehemu ya faradhi, Sala itasihi machoni mwa Allah. Naam, akisahau sehemu iliyo faradhi, lakini akakumbuka baadaye ndani ya Sala ama baada ya Sala, ama alikumbushwa baada ya Sala, hapo mtu huyo anapaswa kutenda hiyo sehemu aliyosahau na pia atafanya sujuda mbili za kusahahu. Sehemu za Faradhi ndani ya Sala ndizo zifuatazo:

1. Takbirah Tahrifah, yaani kutamka Allahu Akbar kwa kuingia katika Sala.

2. Qiyam: Hali ya kusimama wima.

3. Rukuu: Hali ya kuinama.

4. Sajdah: Hali ya kusujudu.

Hizo ndizo sehemu zinazopatikana katika kila rakaa.

5. Qadah ya mwisho: hali ya kuketi katika Rakaa ya mwisho kabla ya kutoa salam kumaliza Sala. Hali hiyo haipo katika kila

Rakaa bali katika Rakaa ya mwisho pekee.

6. Usomaji wa Sura Fatiha: Hiyo nayo ni ya lazima sana katika kila Rakaa.

Imam anaposalisha maamuma, inamlazimu kusoma Sura Fatiha kwa sauti kubwa katika Rakaa mbili za mwanzo za Sala hizi:

- a. Sala ya Alfajiri ambayo ina Rakaa mbili.
- b. Sala ya Magharibi ambayo ina Rakaa tatu.
- c. Sala ya Isha ambayo ina Rakaa nne.

Zingatia: Kama sehemu yoyote ya Quran (zaidi ya sura Fatiha) hazikusomwa katika Rakaa mbili za mwanzo, Sala habatiliki. Lakini mtu akikumbuka kosa hilo hana budi kufanya sujuda mbili za kusahau ili kuirekebisha Sala yake.

Kama Imam akisahau kusoma Sura Faatiha kwa sauti kubwa na pia aya nyingine baada ya Sura Fatiha katika Rakaa yoyote, na akakumbushwa kabla hajaenda katika hali ya Rukuu, anatakiwa kurudia kusoma Sura Faatiha na aya nyinginezo za Quran Tukufu kabla hajaenda katika hali ya Kuinama (Rukuu). Hapo hatatakiwa kufanya sujuda mbili za kusahau.

Lakini kama akiisha waongoza maamuma katika hali ya Rukuu ndipo akakumbuka kosa lake hilo, hapo ye ye hahitaji kurudia Sura Fatiha na aya nyingine za Quran Tukufu. Sujuda mbili za kusahau zitatosha kuirekebisha Sala.

## **WAJIBAAT (SEHEMU ZILIZO WAJIBU) KATIKA SALA**

Wajibaat ni kifungu cha pili. Hizo ni sehemu ambazo mtu akiziaccha kusudi, Sala yake haitasihi. Lakini akiziaccha kwa kusahau kisha akakumbuka baadaye, Hapo mtu anapaswa kufanya sujuda mbili za kusahau kabla ya kutoa salam mwishoni mwa Sala. Sujuda hizo mbili za kusahau zinatosha

kuirekebisha Sala. Sehemu iliyoachika kwa kusahau haina haja tena irudiwe. Wajibaat za Sala ni hizi:

1. Usomaji wa sehemu yoyote ya Quran baada ya kusoma Sura Fatiha katika Rakaa mbili za mwanzo za Sala ya Faradhi na katika Sala nzima za sunnah na nafali.
2. Kusimama wima baada ya Rukuu, iitwayo Qauma katika istilahi. Zingatia ya kwamba Qiyam ni faradhi, lakini Qauma ni Waajib, yaani wajibu.
3. Jilsa, kuketi baina ya sujuda mbili.
4. Kuketi katika Attahiyyatu baada ya kumliza Rakaa ya pili (isiyo Qa'dah ya mwisho).
5. Usomaji wa Tashah-hud, yaani Attahiyyatu Lillahi ... katika hali ya Qa'dah.
6. Kwa Imam kusoma Sura Fatiha na sehemu ya Quran Tukufu kwa sauti kubwa katika Rakaa mbili za kwanza za Sala ya Alfajiri na Magharibi na Rakaa mbili za Isha na Sala ya Ijumaa na Sala za Idi mbili, na usomaji wa hizo kimoyomoyo katika Sala za Adhuhuri na Alasiri.
7. Tartibu, yaani kutimiza sehemu zilizo faradhi na wajibu za Sala kwa mfuatano uliowekwa na dini.
8. Ta'dil. yaani kutimiza sehemu za Sala kwa heshima, adabu na usawa. Ndiyo kusema kwamba Sala isaliwe kwa makini sana kwa kuweka moyo ndani yake bila kusali haraka haraka.
9. Kutoa salamu kulia na kushoto kwa kusema Asslaamu alaikum wa Rahmatullah kwa kuonyesha kwamba Sala imekwisha.
10. Kwa Imam, kutamka Takbira Tahrim kwa sauti kubwa.

## SUNNA ZA SALA

Sehemu nyingine zote minghairi ya faradhi na wajibu ndiyo Sunna na Mustahab. Mwenye kusali ashikamane sana na sunna na mustahab pia bila kuziacha pasipo sababu maalum. Hata hivyo, sujuda mbili za kusahau hazina haja kama sehemu yoyote iliyo sunna ama mustahab imeachika. Sehemu zilizo sunna za Sala ndizo zifuatazo:

1. Kunyanya mikono hadi ndewe za masikio wakati wa kutamka Takbira Tahrим.
2. Kufunga mikono katika Qiyam.
3. Kusoma thanaa.
4. Usomaji wa A'uudhu billahi minash-shaitanir-Rjiim kabla ya kusoma Sura Fatiha.
5. Kutamka Aamiin mwishoni mwa Sura Fatiha.
6. Kutamka Takbira kabla ya kwenda katika Rukuu.
7. Kusema Subhaana Rabbiyal Adhiim mara tatu katika Rukuu.
8. Kusema Sami'allaahu Likan Hamidah wakati wa kuinuka kutoka katika Rukuu, na kama mtu akisali peke yake, kusema Rabbanaa walakal Hamdu. Kama mtu yu maamuma akisali nyuma ya Imam kusema Rabbanaa walakal Hamdu ndiyo sunna ya Mtume Mtukufu s.a.w.
9. Kutamka Takbira kabla ya kwenda katika hali ya kusu-judia.
10. Usomaji wa Subhana Rabbiyal A'laa mara tatu katika sujuda.
11. Kuomba dua iliyofundishwa iombwe katika Jilsa.
12. Kuinua kidole cha shahada wakati wa kusema Ash-hadu allaa ilaaha illallaah....
13. Sala ya Mtume na maombi mengine katika Qa'dah ya mwisho.
14. Usomaji wa Sura Fatiha katika rakaa ya tatu na ya nne.
15. Kwa Imam: Kutamka Takbira na kusema Samiallahu liman hamidah kwa sauti kubwa inayosikika kwa maamuma.

## **MUSTAHABBAT ZA SALA**

Mambo yanayopendeza ndani ya Sala yaitwa Mustahabbat za Sala. mambo hayo si ya lazima sana wala siyo sehemu zinazoitwa sunna, lakini ni mazuri na ya kupendeza, na ndiyo haya yafuatayo:

1. Kuangalia katika Sala pale pa kusujudia.
2. Kuweka mikono juu ya magoti kwa kuvitenganisha vidole visigusane katika hali ya Rukuu.
3. Kunyosha mikono ikining'inia ubavuni katika hali ya Qauma.
4. Kusujudia kwa namna ambavyo magoti yaguse chini kwanza, kisha mikono, tena pua na paji la uso.
5. Kuinuka kutoka sujuda baada ya kumaliza Rakaa ya pili pasipo msaada wa kitu.
6. Kuweka mikono mapajani karibu na magoti kwa kuvitawanya vidole vikielekea kibla katika hali ya kukaa katika Attahiyyatu.
7. Kukaa juu ya mguu wa kushoto katika Qa'dah na Jilsa na kusimamisha mguu wa kuume namna ambavyo vidole vya mguu huo vielekee kibla.
8. baada ya sura Faatiha, zile aya zinazoongezwa katika Rakaa ya kwanza ziwe nyingi kuliko zile zinazoongezwa katika Rakaa ya pili.
9. Kwa maamuma: Kusema Aamiin kwa sauti inayosikika na kusema Rabbanaa wa lakal Hamdu kimoyomoyo.

## **MAKRUHAAT ZA SALA**

Mambo yasiyopendeza ndani ya Sala yaitwa Makruhaat za Sala. Mtu anapaswa kusali akizingatia kwamba amesimama mbele ya Mola wake. Makruhaat ni hizi zifuatazo:

1. Kuchezacheza na mavazi uliyovaa.
2. Kutazama kulia, ama kushoto, au kutazama juu mbinguni.
3. Kufumba macho.
4. Kusali pasipo kufunika kichwa.
5. Kutokuelekeza vidole vya miguu kwenye kibla katika hali ya sujuda, ama kunyanya juu miguu katika hali ya kusujidia.
6. Kuanza kusali wakati mtu anasikia njaa sana, huku chakula kimeandaliwa.
7. Kuendelea na Sala wakati mtu anasikia sana haja ya kwenda msalani.
8. Kusali katika uwanja wa makaburi kwa kuelekea kaburi.
9. Kusali kwa kuvala nguo za kubana sana hata mtu anaona shida kusali.
10. Kusali mahali pasipofaa kama vile katika zizi la farasi, ng'ombe, mbuzi ama soko lenye makelele.
11. Kusimama kwa kuweka uzito kiwiliwili juu ya mguu mmoja ama kufanya yaliyo kinyume na heshima na adabu ya kusali.
12. Kusali mahali pa wazi pasipo kuweka Sutra. Sutra ni kitu kinachowekwa mbele kwa kuonesha eneo la mwenye kusali, ili mtu ye yeyote humo kwa maana atavuruga Sala yake.
13. Kutingisha kichwa wakati mtu ye yeyote akisema Assalaamu Alaikum.
14. Kusali pasipo kusafisha kinywa baada ya kula.
15. Kugeuza mfuatiliano wa Sura. Yaani kusoma Sura andamizi (mfano: Sura An-Nasr) katika Rakaa ya kwanza na kusoma Sura tangulizi (mfano: Sura Al-Kauthar) katika Rakaa ya pili.

16. Kuweka mikono chini ya paji la uso katika hali ya sajdah.
17. Kuweka tumbo juu ya kitu kingine wakati wa kusujudia.
18. Kutandaza chini mikono hadi viwiko katika sujuda.
19. Kusoma aya za Qurani Tukufu katika sujuda.
20. Kumtangulia Imam, yaani kufanya haraka na kuingia katika sehemu ya mbele ya Sala kabla ya Imam.

**Ukumbusho 1:** Mwenye kusali anaweza kumwondoa ama kumwua mdudu mwenye kudhuru akimkuta karibu naye ndani ya Sala.

**Ukumbusho 2:** Mahali pa kusalia pawe safi, na hewa iwezekanavyo isiwe na harufu mbaya. Kila Mwislamu anapaswa kuiheshimu Sala hata kama mwenyewe hayumo ndani ya Sala. Mtu yejote asimtatize mwenye kusali kwa matamshi ama kwa kitendo kingine cha kumvurugia utulivu wake. Ndiyo sababu hakuna ruhusa kupita mbele ya mwenye kusali isipokuwa kwa kuliacha eneo lake anamosalia. Ndiyo kusema kwamba mtu anapaswa kungoja na kusubiri asipite mbele ya mwenye kusali hadi mwenye kusali awe amemaliza Sala yake kwa kutoa salamu.

## MAMBO YANAYOVUNJA SALA

Mambo yafuatayo hayalingani na usahihi wa Sala na yanayunjilia mbali Sala ya mtu yakinendeke:

1. Udu unapotanguka.
2. Kula na kunywa mtu akiwa anasali.
3. Kuzungumza ama kumwitikia mwengine ilhali unasali.
4. Kucheka ndani ya Sala.
5. Kuelekeza uso kulia ama kushoto unaposali.

## **SUJUDUS-SAHWI (SUJUDA ZA KUSAHAU)**

Kama mtu anatenda kosa ndani ya Sala ambalo linaiathiri Sala yake, hapo anatakiwa kufanya sujuda mbili za kulirekebisha kosa hilo. Kwa mfano akiwa na shaka kwamba amesali idadi sawasawa za Rakaa ama amezipunguza ama ameziongeza, hapo atafanya sujuda mbili za kusahau.

Sujuda hizo mbili zinafanywa baada ya Tashah-hud , Sala ya Mtume na maombi mengineyo katika Qa'dah ya mwisho ya Sala na kabla hajatoa salam. Imam akitamka takbira anakwenda katika sujuda ambao anasema subhaana Rabbiyal A'laa mara tatu. Kisha akitamka Takbira anakaa, na hapo anatamka Takbira tena na anafanya sujuda ya pili kama ile ya kwanza. Ndipo anatamka tena Takbira na kukaa katika Qa'dah na bila kusema chochote kingine anatoa salam kulia na kushoto kama kawaida ili kumaliza Sala yake.

Kama Imam anafanya kosa linaloweza kurekebishwa na sujuda mbili za kusahau, hapo maamuma wote nao wanapaswa kufanya sujuda mbili pamoja na Imam. Lakini maamuma mmojawapo akitenda kosa, yeye huyo maamuma hatafanya sujuda za kusahau.

Kama kuna shaka kuhusu idadi ya Rakaa zilizosaliwa, hapo kanuni ya uyakini inashikwa. Yaani kama kuna shaka kwamba umesali Rakaa tatu ama nne, hapo tatu bila shaka umesali, na shaka imo katika ile ya nne kwamba umesali ama hukusali. Hapo unatakiwa kuongeza Rakaa moja ikiwa ya nne uliyo na shaka nayo kwamba ulisali ama hapana.

## **SALA YA MGONJWA**

Kusali ni jambo la muhimu kabisa katika Islam. Mgonjwa asiyeweza kusimama kusali anatakiwa asali akikaa. na kama hawezi hata kukaa, hapo atasali akilala. Kama hawezi kuianama katika Rukuu au hawezi kufanya sujuda kwa sababu ya maradhi, ye ye anaruhusiwa kufanya ishara ya kuinama ama kusujudia. Na kama yu mgonjwa sana hadi hawezi hata kutikisa kichwa ama mikono, hapo anapaswa kunuia na kuwaza moyoni kwamba anainama na anasujudia au anafunga mikono na kadhalika.

## **SALA KATIKA HALI YA SAFARI**

Kama mtu anasafiri kwa njia ya usafiri inayomzuia asiweze kusimama ama kutoka nje na kusali, ye ye mtu huyo anaweza kusali ndani ya gari akikaa mahali pake wala hatalazimika kuelekeza uso wake kwenye kibla katika hali hiyo maana haiwezekani. Anaweza kusali akielekeza uso wake upande anapoenda farasi wake ama gari au jahazi, ndege na kadhalika, ikiwezekana. Katika siku za mwanzoni za Islam, Sala za Adhuhuri, Alasiri na Isha zinazosaliwa pamoja na jaama zilikuwa za Rakaa mbili za faradhi kama Sala ya Alfajiri, lakini hapo baadaye hizo Rakaa mbili zilibakia kwa Sala hizo katika hali ya safari pekee. Katika hali ya kawaida Sala hizo zikawa za rakaa nne kila moja. Kwa hiyo sasa kikawaida mtu anapaswa kusali Rakaa nne za Adhuhuri na nne za Alasiri asipokuwa safarini; lakini katika hali ya safari atasali Rakaa mbili za Adhuhuri na mbili za Alasiri na mbili za Isha.

Kama msafiri anafikia mahali ambapo ye ye anataka kukaa siku chache kuliko 15, ye ye atatakiwa kusali Sala ya safari. lakini kama ananuia kukaa hapo siku 15 ama zaidi, hapo atasali Sala

kamili tangu siku ya kwanza ya kufikia hapo.

Hata hivyo, haruhusiwi kupunguza Rakaa za Sala za faradhi za Alfajiri na Magharibi.

Kama mtu yu mgeni kwa jamaa yake wa karibu ambaye nyumba yake anaihesabu kuwa nyumba yake mwenyewe, kama vile nyumbani kwa wazazi wake, ama kwa wakwe zake au kama amekwenda katika makao makuu ya kidini kama vile Makkah, Madina, Qadian aua Rabwa na kadhalika, hapo pia anaweza kupunguza Sala yake na kusali Sala ya safari, lakini ni bora asali Sala kamili bila kupunguza, yaaani Rakaa nne badala ya mbili.

Mtu akiwa safarini, sehemu ya Sala iliyo sunna haisaliwi, isipokuwa Rakaa tatu za witri na Rakaa mbili za sunna za Sala ya Alfajiri.

Kusali Sala za nafali katika hali ya safari ndiyo hiari ya mtu kabisa.

Isitoshe, mtu anaruhusiwa kukusanya Sala mbili katika safari. Sala ya Adhuhuri inaweza kukusanywa na Sala ya Alasiri. Sala hizo mbili zaweza kusaliwa pamoja wakati wa Sala ya Adhuhuri ama wakati wa Sala ya Alasiri. kadhalika Sala ya Isha inaweza kukusanywa pamoja na Sala ya Magharibi katika wakati wa Magharibi ama wakati wa Isha.

Kama wasafiri wanasali nyuma ya Imam ambaye ni mkazi, hapo wasafiri watatakiwa kumfuata Imam na kusali pamoja naye Rakaa nne za Adhuhuri, nne za Alasiri na nne za Isha. Hapo sheria ya kupunguza Sala haitatumika. Lakini kama Imam ndiye msafiri, ye ye anapunguza Sala yake kama ilivyo sheria na wasafiri walio nyuma yake pia watapunguza Sala zao na watatoa salamu pindi Imam anapotoa salamu kumaliza Sala. Lakini wasio safarini, bali ndio wakazi, hawatatoa salamu pamoja na Imam, bali watainuka Imam akiisha toa salamu, na kukamilisha Sala zao.

## **SALA WAKATI WA HATARI (SALATUL-KHAUF)**

Inaruhusiwa kupunguza Sala katika hali ya hatari ya kufa, kama vile vita. Sala katika hali ya hofu ya aina hiyo yaweza kusaliwa kwa njia kumi na moja mbalimbali ilivyoelezwa katika Quran Tukufu na Hadithi. Kiini hasa cha habari hii ni kwamba kama vita kali inaanza katika uwanja wa vita, au kama mtu anatazamia kwamba maadui watashambuli ghafla, au kama wanajeshi wamelazimika kushika mahali pao katika mahandaki, hapo Sala zaweza kufupishwa ama kupunguzwa kwa sababu ya hali ya hatari. Kama ipo nafasi ya kusali Rakaa mbili, asali Rakaa mbili, la sivyo hata Rakaa moja itakubaliwa. kama kusali pamoja nyuma ya Imam ni jambo la hatari, kila mmoja atasali peke yake mahali alipo, na kama hali iko mbaya zaidi, mtu anaweza kusali akitembea kwa miguu au juu ya mnyama, gari n.k., bila kujali anaelekea kibla ama hapana. Na kama hatari ni ya kufa na kupona, Sala zinaweza kusaliwa kwa ishara ama kwa kunuia tu pamoja na kusoma baadhi ya maneno maalum ya Sala. Pia iko ruhusa kukusanya Sala nyingi pamoja katika hali ya hatari kama hiyo. (Bukhari, Kitabul Maghazi, Bab Ghazwah Khandak, Muslim Kitabus Salaah, Baab Salatil-Khauf).

## **QADHA AMA KUKIDHI SALA**

Kama mtu hakuwahi kusali Sala fulani katika wakati wake kwa sababu alisahau au alien dela kulala au kuzimia na kadhalika, Sala hiyo atakaposali baadaye inaitwa Sala ya Qadha, yaani kukidhi ama kulipa Sala. Mtu anatakiwa kusali ile sehemu ya Sala iliyo ya faradhi wakati wa kukidhi Sala iliyokwisha pita wakati wake. Mtu akikumbuka tu ile Sala au zile Sala asizowahi kusali katika nyakati zake, anatakiwa azisali mara moja bila kukawia sawa na mpango wa kawaida wa hizo Sala, yaani

kwanza Sala ya Adhuhuri, kisha Alasiri na hapo baadaye Magharibi na kadhalika.

Baadhi ya viongozi wa dini wametoa fatwa kwamba mtu anaweza kusali Sala moja pekee kwa kulipa Sala zote za maisha mazima. Wamezua istilahi ya "Qadha Umri" kwa kitendo hicho. Kwa sababu hiyo watu wamekuwa wazembe, hawajibidiishi kusali.

Sala ni chakula cha roho cha kila siku. Inawezekana kwamba mtu asile kwa miaka kumi akisikia njaa kisha akile chakula cha miaka kumi mara moja katika wakati mmoja. Ni kuharibia umuhimu wa Sala kushauri kwamba mtu anaweza kughafilika kutimiza faradhi yake ya kusali maisha mazima, kisha siku moja asali Qadha Umri kulipa Sala zote zile za maisha yote. Hilo silo fundisho la Mtume Mtukufu wa Islam s.a.w.

Sawa na fikha ya Kiislamu, kama mtu ameacha hata Sala moja kwa makusudi, Sala hiyo imekwisha potea kwa kudumu wala haiwezi kulipwa kabisa. Naam, Mwenyezi Mungu ndiye mwamuzi wa kweli kuhusu habari hii. Mtu huyo anatakiwa atubu kwa moyo wote na kwa unyenyekevu kwamba hatarudia kosa kama hilo tena maisha yake mazima.

## **SALA YA TAHAJJUD**

Kulala mapema baada ya Sala ya Isha na kuamka kwa ajili ya Sala ya nafali ya Tahajjud katika sehemu ya mwisho ya usiku kabla ya kupambazuka ni chanzo cha baraka nyingi. Ijapokuwa hiyo siyo Sala ya faradhi, lakini imesisitizwa sana ndani ya Quran Tukufu. Ni desturi ya siku zote ya watawa kusali Sala hiyo kila siku ili kujipatia fadhili maalumu za Allah. Wakati wa Sala ya Tahajjud unamalizika ambapo saa ya kusali Alfajiri inaanza. Dua zinazombwa katika Sala ya tahajjud hupokelewa kwa

haraka zaidi. Hii ndiyo njia ya kujipatia ukaribu na Allah, kwani katika saa kama hizo mtu anauacha usingizi wake na hajali raha yake ya kulala ili aangukie kifudifudi na kusujudia mbele ya Mola wake. Sala ya tahajjud inazo Rakaa nane. Mtume Mtukufu s.a.w. siku zote alisali Sala ya Tahajjud kwa kuigawa katika Rakaa mbilimbili. Yaani baada ya kila Rakaa mbili akatoa salamu, na kwa njia hiyo alikamilisha kwa jumla Rakaa nane. Mtume s.a.w. alikuwa anasoma sehemu ndefu sana za Quran Tukufu katika Qiyam na alikuwa anakaa katika Rukuu kwa muda mrefu zaidi na pia sujuda zake zilikuwa ndefu sana, akiomba maombi mengi mengi. Yeye alikuwa anazifuatisha Rakaa tatu za Witri mara baada ya Sala ya tahajjud. Hivyo, yeye alikuwa anasali Rakaa kumi na moja kila siku kabla ya kupambazuka.

## SALA YA TARAWEHE

Sala ya tarawehe (Tarawiih kwa Kiarabu) ni Sala maalum inayosaliwa katika mwezi wa ramadhan kila siku wakati wa usiku. Hasa Sala hiyo husaliwa katika saa za Tahajjud, yaani ndiyo Sala ya Tahajjud yenyewe ambayo Hadhrat Umar r.a. katika zama za Ukhilifa wake aliruhusu iweze kusaliwa mara baada ya Sala ya Isha katika mwezi wa Ramadhan ili kuwawezesha wale wasio-weza kwa sababu hii au ile kuisali katika saa za Tahajjud. Hata hivyo ni afadhali kuisali katika wakati kabla ya kupambazuka Alfajiri. Desturi ya Waisalmu ndiyo kusoma sehemu ndefu zaidi za Quran Tukufu katika Sala ya Tarawehe kwa kuifuata kawaida ya masahaba wa Mtume s.a.w.

Sala ya tarawehe inazo rakaa nane. lakini mtu anaweza kuzisali Rakaa nyingi zaidi kama vile ishirini ama zaidi. Baada ya kila Rakaa nne kupumzika kwa kitambo kidogo ndiyo sawasawa.

## **SALA YA KUPATWA JUA NA MWEZI**

Kupatwa jua huitwa Kusuf na kupatwa kwa mwezi huitwa Khusuuf. Badiliko hili la jua na mwezi kupungukiwa mwanga wakati wa kupatwa humkumbusha muumini kwamba kama vile sayari hizi zinapopatwa huonekana kupoteza sana nuru zao, ndiyo ziwezavyo dosari kadha wa kadha za kiroho kupunguza ile nuru ya kiroho inayoungaza moyo wake. Allah pekee anaweza kumkinga mtu asipatwe kiroho. Kwa hiyo, Sala maalum ya Rakaa mbili imeagizwa wakati wa kupatwa jua na mwezi ili kuwazindua waaminio kwamba wajitafutie baraka za Allah na kupata huruma yake ikiwa wanataka kunyanyuka kiroho.

Wakazi wa mji au kijiji wanasali Rakaa mbili ndani ya msikiti au mahali pengine pa wazi nyuma ya Imam. katika Sala hii baada ya Sura Fatiha, sehemu ndefu za Quran Tukufu zinasomwa kwa sauti kubwa. Kila rakaa ina Rukuu mbili. Yaani baada ya kusoma sura Faatiha na sehemu nyingine ndefu ya Quran Tukufu, Rukuu inafanywa, na baada ya Rukuu Imam anapoinuka katika Qiyam haendi katika sujuda bali anaanza tena sehemu nyingine zaidi ya Quran Tukufu na kisha kuinama tena katika Rukuu ya pili. Sawa na masimulizi mengine Mtume s.a.w. penigne alifanya Rukuu tatu pia katika rakaa moja. Kishapo Imam anakwenda katika sujuda. maombi mengi mengi yanaombwa katika Rukuu za Sajdah pia. Baada ya Sala Imam anatoa hotuba ambamo anapaswa kuwaeleza watu kumwomba Allah msamaha na kuwaambia njia ya kurekebisha hali ya jamaa kwa ujumla.

## **SALATUL-ISTISKAA (SALA YA KUOMBAA MVUA)**

Kama mvua inakosekana kwa muda mrefu, watu wanapaswa kuvutia huruma ya Allah kwa njia ya kusali Salatul-Istiskaa.

Sala hiyo inasaliwa katika mahali pa wazi katika nyakati za mchana. Imam ajivalie shuka moja juu ya nguo zake za kawaida na aanze kusalisha Rakaa mbili kwa njia ya kawaida. Usomaji wa Quran katika Sala hii huwa kwa sauti kubwa wanayosikia maamuma. Baada ya kusalisha Imam anapaswa kuwaongoza watu katika maombi kwa kuinua mikono na kuomba:

اللَّهُمَّ اسْقِنَا فِي شَأْنًا مُّعِيشًا مِّثْلًا مَّا فِي أَعْيُنِنَا فَنَارٌ - عَاجِلًا  
فَنَارٌ عَاجِلٌ - اللَّهُمَّ اسْقِنِ عِبَادَكَ وَبِهَا تُمُكَّ وَالشُّرُّ رَحْمَتَكَ وَ  
أَجْنِي بِنَدَدَكَ الْعَيْنَ طَالَلَهُمَّ اسْقِنَا اللَّهُمَّ اسْقِنَا اللَّهُمَّ اسْقِنَا - هـ

**Matamshi:** *Allahummas-qinaa ghatham-mughitham-murian, naafian ghaira dhaarrin, 'aajilan ghaira aaajilin. Allahummaski 'ibaadaka wa bahaaimaka; wanshur Rahmataka; wa ahyi baladakal-mayyit. Allahummasqinna, Allahummas-qinaa, Allahummasqinaa.*

**Tafsiri:** Ee Allah, tupatie mvua nyingi iletayo rutuba, ifaayo isiyo na madhara, haraka pasipo kukawia. ee Allah, wanyweshe watu wako na wanyama wako na eneza rehema yako, na ihuishe nchi yako iliyokufa. Ee Allah tunyweshe, Ee Allah tunyweshe, Ee Allah tunyweshe.

Kisha Imam amsalie Mtume s.a.w. na azidi kuomba kwa kujinyenyekeza na kumtukuza Allah. Kisha apindue shuka yake aliyojivalia na kuifanya sehemu ya ndani iwe nje na ile ya nje iwe ndani. Hiyo ni namna ya kusema kwamba jinsi shuka hiyo imepinduka kadhalika na Mungu aipindue hali ya watu waliyo nayo kwa sababu ya kukosekana mvua na kubadili kabisa kwa kuwaletea mvua kuwaondolea shida na taabu yao.

## SALATUL-ISTIKHARA

Sala hii inasaliwa kwa kumwomba Allah heri na mwongozo wakati mtu anapotaka kufanya kazi muhimu sana, kama vile biashara, safari, kufunga ndoa na kadhalika. Kazi yenyewe inaweza kuwa ya kidini ama ya kimaisha. Shabaha ya Sala hi ni kumwomba Allah msaada ili mtu afaulu katika shabaha yake.

Sala ya Rakaa mbili inasaliwa kabla ya kwenda kulala usiku. Baada ya sura Fatiha, husomwa sura Al-Kafiruun, katika rakaa ya kwanza, na katika rakaa ya pili, baada ya sura fatiha, Sura Ikhlaas inasomwa. katika Qa'dah baada ya kumaliza Tashahud, Sala ya Mtume na maombi mengine, dua hii ifuatayo inaombwa kabla ya kutoa salam:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْتَخِرُكَ بِقُدْرَتِكَ  
وَأَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ الْعَظِيمِ ، فَإِنَّكَ تَعْلَمُ وَلَا أَعْلَمُ  
وَتَعْلَمُ وَلَا أَعْلَمُ وَإِنَّكَ عَلَيْهِ الْغُرُوبُ ، اللَّهُمَّ إِنِّي كُنْتُ تَعْلَمُ  
أَنَّ هَذَا الْأَمْرَ خَيْرٌ لِّي فِي دِينِي وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أُمْرِي  
فَاقْبِرْزْ لِي وَرَبِّرْ لِي ، ثُمَّ بارِكْ لِي فِيهِ  
وَإِنِّي كُنْتُ تَعْلَمُ أَنَّ هَذَا الْأَمْرَ شَرٌّ لِّي فِي دِينِي وَمَعَاشِي وَعَاقِبَةِ أُمْرِي  
فَاضْرِفْهُ عَلَيْيَ وَاضْرِفْنِي عَنْهُ وَاقْبِرْ لِي الْخَيْرَ حَيْثُ كَانَ ثُمَّ أَرْضِنِي بِهِ

**Matamshi:** *Allahumma inni astakhiruka bi-ilmika, wa astaqdiruka bi-qudratika, wa as'aluka min fadhlikal Adhiim. Fa-innaka taqdiru wala aqdiru, wa ta'lamu walaa a'lamu, wa anta 'allaamul-ghuyuub. Allahumma inkunta ta'lamu anna hadhal-amra khairullii fidini wa ma'ashi wa aaqibati amrii, faqdirhu lii wa yassirhu lii, thumma baarik li fihi. Wa inkunta ta'lam anna hadhal-amra sharrulii fii diinii wa ma'ashi*

*wa aaqibati amri fasrifhu anni, wasrifni anhu. Waqdir liyal khaira haithu kaana, thumma ardhinii bihi.*

**Tafsiri:** Ee Allah, nakuomba heri kwa elimu yako, na nakuomba uwezo kwa uwezo wako, na ninakuomba fadhili yako kubwa. Kwani unaweza nami siwezi, na unajua nami sijui, nawe u mjuzi wa mambo ya ghaibu. Ee Allah, kama katika ujuzi wako kazi hii ndiyo heri kwangu katika dini yangu na maisha yangu na mwisho wa jambo langu, basi niwezehse hiyo na nirahisishie hiyo, kisha itilie baraka kwa ajili yangu. na kama katika ujuzi wako kazi hii ndiyo shari kwangu katika dini yangu na maisha yangu na mwisho wa jambo langu, basi Uiweke mbali nami, na niweke mbali nayo. na Nikadirie heri popote ili[po, kisha niridhishe nayo. (*Bukhari, Kitaabud-Da'waat, Baabud-Dua indal-istikhara*).

## SALATUL HAJAH (SALA KATIKA WAKATI WA HAJA)

Sala hii insaliwa wakati mtu anapokuwa katika shida fulani na anahitaji msaada wa Allah. Mtume Mtukufu s.a.w. alisema ya kwamba kama kuna mtu ambaye anahitaji kitu fulani, yeye mtu huyo atawadhe na kisha asali Rakaa mbili. Katika Rakaa ya pili ndani ya Qa'dah ya mwisho, baada ya kusoma Tashahhud, Sala ya Mtume na maombi mengine ya kawaida, amsifu Allah na kumsalia Mtume s.a.w. na kisha kabla ya kujtoa salamu aombe dua ifuatayo. Yatumainiwa Mungu atamfungulia njia ya kupata shabaha yake:

رَبِّ الْأَنْشَاءِ إِلَّا إِنَّهُ الْعَلِيُّمُ الْكَرِيمُ. سُبْحَانَ اللَّهِ رَبِّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ. الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ. أَسْتَأْلُكَ مُؤْجِبَاتِ رَحْمَتِكَ وَغَزَائِمَ مَخْفَرِكَ وَالْغَيْمَةَ مِنْ كُلِّ بَرِّ وَالسَّلَامَةَ مِنْ كُلِّ إِثْمٍ. لَا تَذَرْعُ لِيْنِ ذَنْبِ الْأَعْفُونَهُ وَلَا حَمْمَأَ الْأَفْرَجَتَهُ وَلَا حَاجَةَ حِنْ لَكَ رَضِيَ الْأَقْبَيْتَهُ لَيَا أَرْحَمَ الرَّاجِهِنَ.

**Matamshi:** *La ilaaha illallaahul-haliimul-Kariim, Sub-haanallahu Rabbil Arshil-Adhiim. Alhamdulillaahi Rabbil-A'lamiin. As'aluka muujibaati rahmatika, wa 'azaaima maghfiratuka, wal-ghanimata min kulli birrin, was-salaamata min kulli ithmin. La tada' lii dhamban illaa ghafartahu, wala hamman illa farrajtahu, wala hajatan hiya laka ridhaa illa qadhitaha, Ya Arhamr-Raahimiin.*

**Tafsiri:** Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah, Mpole, Mkarimu. Utukufu ni wa Allah, Mola wa Arshi Kuu, Sifa zote njema zinamhusu Allah. Nakuomba yale yanayosababisha rehema yako kuja na yale yanayovutia maghufira yako na mengi kutokana na kila wema na usalama katika kila dhambi. Usiniachie dhambi kwangu isipokuwa uisamehe, wala shida isipokuwa Uiondowe, wala haja unayoiridhia isipokuwa Uitimize, Ee Allah Mwenye rehema nyingi zaidi kuliko wenye rehema wote.

## SALA YA ISHRAAQ

Sala hii ya nafali ina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni kusali rakaa mbili kitambo kidogo baada ya jua kuchomoza. Na sehemu ya pili ni kusali Rakaa nne ama nane wakati jua linapokuwa juu zaidi kama vile asubuhi saa tatu hivi. Sehemu ya kwanza ya Sala hiyo inaitwa Salatul-Ishraaq na sehemu ya pili Salatudh-Dhuhaa. Hiyo pia imeitwa Salatul -Awwabiin.

Katika baadi ya Hadithi hata hivyo rakaa sita zinazosalihwa baiana ya Sala ya Magharibi na Isha huitwa Salatul-Awwabiin.

## SALAT-US-TASBIH

Sawa na matamshi ya Mtume Mtukufu s.a.w. yejote mwenye kusali Salatu Tasbihi hupata thawabu nyingi toka kwa Allah. Hii ni Sala ya Nafali yenye rakaa nne ambayo sawa na maisha ya mtu, yaweza kusaliwa mara moja kila siku, au mara moja kwa wiki au mara moja kwa mwaka au hata mara moja katika maisha ya mtu. Sala hii yaweza kusaliwa wakati wowote ule minghairi ya nyakati zilizokatazwa kusali.

Katika kila Rakaa, baada ya kusoma Sura Fatiha na aya nyaginezo za Quran Tukufu, haya yafuatayo hurudiwa mara kumi na tano:

**سُبْحَانَ اللَّهِ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ وَلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ**

**Matamshi:** *Subhaanallahi wal Hamdulillaahi walaa ilaaha illallahu wallahu Akbar.*

**Tafsiri:** Allah ndiye asiye na makosa na sifa zote njema zinmhusu Allah. Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah na Allah ni Mkuu kuliko kila kitu.

Maneo hayo hayo pia yanarudiwa mara kumi katika sehemu zifuatazo za Sala:

- Rukuuu, baada ya kusema Subhaana Rabbi yal Adhiim.
- Qauma, baada ya kusema Samia Allahu liman Hamidah na Rabbanaa wa lakal Hamdu.
- Sajdah, Katika mara zote mbili za kusujudu baada ya kusema Subhaana Rabbi yal A'alaa.
- Jilsa, baada ya kuomba dua ya sehemu hii ya Sala.
- Qa'dah, baada ya kuomba dua ya sehemu hii ya Sala

Hivyo basi, mtu atayarudia hayo yaliyotajwa hapo juu mara 75 katika Rakaa moja na mara mia tatu katika Rakaa nne za Sala hiyo. Hii yamaanisha kwamba Qa'dah inakuwa sehemu ya kila Rakaa pamoja na Rakaa ya kwanza na ya tatu.

Kuhusu Sala za nafal, mtu anapaswa kufahamu ya kwamba Sala hizo ni za daraja la pili. Sala za faradhi ndizo zenye umuhimu zaidi sana. Isitoshe, mtu anaweza kujifaidisha na Sala za nafali hapo tu ambapo mtu amekwisha timiza wajibu wake kumhusu Allah na wanadamu wenzake.

## SALA YA JENEZA

Inapooneka kwamba mtu fulani ni karibu na kufa, hapo usomaji wa Sura Yasin (Sura ya 36 ya Quran tukufu) karibu naye hupendekezwa. sababu hasa ya kusoma Sura hiyo ni kwamba katika sura hiyo madhumuni iliyoelezwa ni ya namna ambayo itamburudisha kiroho na kumwondolea mbali shida za mauti. Pia isomwe kalima Tayyiba na shahada mbili kwa sauti ndogo karibu na huyo aliyekurubia kufa. Na mtu anapokuwa, hapo watu wote waliopo hapo na wengine nao waliopo hapo na wengine nao wanaopata habari ya kifo wanapaswa kutamka:

**إِنَّا إِلَيْهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ**

**Matamshi:** *Inna lillaahi wa innaa ilaihi Raji'uun.*

**Tafsiri:** Hakika sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Macho ya marehemu yafumbwe kwa mkono na kitambaa kifungwe pembeni mwa kidevu na kichwa ili kinywa kisibaki wazi. Badala ya kuomboleza mtu anapaswa kuonesha subira na kwa makini ashughulikie matayarisho ya mazishi. Maiti ioshwe kwa njia ifuatayo:

Maji ya kawaida ama yaliyo ya uvuguvugu, ya moto kidogo, yatumiwe kwa kuosha maiti mara tatu. Mtume Mtukufu s.a.w. alikuwa na desturi ya kutia majani ya mkunazi katika maji ya

kuosha maiti, kwani majani hayo yanaua vijidudu. kwanza kabisa, zile sehemu za maiti zioshwe ambazo zinaoshwa wakati wa kutawadha, ijapokuwa haina haja ya kutia maji kinywani wala puan kwa kuvisafisha wala haina haja ya kuosha miguu. Kisha mwili unaoshwa, kuanzia upande wa kuume na kisha upande wa kushoto uoshwe. Sehemu zake za siri ziwe zinafunika kwa kitambaa kama kawaida. wanaume pekee wanaweza kuosha maiti za kina mama. Mwili baada ya kuoshwa uvishwe sanda ambayo hutengenezwa kutokana na kitambaa cheupe kisicho ghali.

sanda ya mwanamume ni shuka tatu: shuka ya kifuani, shuka ya kiunoni na shuka ya kufunikia mwili mzima gubigubi. Kwa maiti wa kike vitambaa viwili vinaongezwa, kimoja badala ya sidiria na kingine kama shungi.

Islam inafundisha kufanya matayarisho ya mazishi kwa njia ya kawaida isiyo ya kujifaharisha.

Mtu aliyeuawa katika njia ya Allah (Shahiid) hana haja ya kuoshwa wala kuvishwa sanda. Anapaswa kuzikwa katika nguo zake alizokuwa amezivaa wakati wa kuuawa.

Baada ya kuoshwa na kuvishwa sanda, jeneza linapelekwa juu ya mabega pale ambapo maiti itasaliwa. Sala ya maiti hu-saliwa katika mahali pa wazi au palipojengwa kwa shabaha hii. Waliohudhuria kusali wanapaswa kusimama katika safu nyuma ya Imam. Idadi ya safu iwe witri yaani idadi isiyogawanyika sawasawa na 2. Imam anasimama mbele kabisa ya safu ya kwanza, katikati ya safu, na mbele yake kuna maiti. mwili wa maiti uwekwe namna ambavyo upande wa kuume wa maiti uwe upande wa kibla.

Imam anaongoza Sala ya maiti kwa kutamka Takbir, Allahu Akbar, yaani Allah ni Mkuu kuliko vyote, kwa sauti kubwa wanayosikia maamuma. Maamuma nao wanatamka Takbir lakini kwa sauti ndogo, kimoyomoyo. Kisha Imam anasoma Thanaa na sura Faatiha kimoyomoyo. Kisha anatamka takbir

tena pasipo kuinua mikono juu; mikono itaendelea kufungwa kifuani. Maamuma nao watamuata Imam katika yote hayo. Kisha wote, maamuma pamoja na Imam, watamsalia Mtume s.a.w. kimoyomoyo. Hapo tena Imam anatamka Takbira ya Tatu inayosikika kwa maamuma na kisha anasoma dua maalum iliyofundishwa kuombea maiti, ambayo tutaiandika hapa chini baada ya kueleza mengine machache. Kisha Imam anatamka tena Takbira ya nne na anatoa salamu kulia na kushoto kwa kusema Assalaamu Alaikum Warahmatullah kuonesha kwamba Sala ya maiti imekwisha.

Maamuma nao watamuata Imam katika hayo yote na kutamka Takbira ya nne na kutoa salamu kulia na kushoto kama kawaida.

Zingatieni kwamba katika Sala ya maiti hakuna Rukuu wala sujuda, wala hamna adhana wala iqamah.

Sala ya maiti inaweza kusaliwa pia ilhali maiti haiko pale. Hii mara nydingine hufanywa kwa marehemu watukufu ama marehemu ambaye hakupata watu wengi kumsalia. Kumsalia maiti ni faradhi ya waislamu wote kwa jumla. Na baadhi ya Waisalmu wakiisha msalia maiti, itahesabiwa kwamba walimsalia kwa niaba ya Waisalmu wote kwa jumla. Hiyo inaitwa Fardh Kifaya.

Kama maiti ni mwanamume au mwanamke aliyebalehe, dua hii itaombwa baada ya kutamka ile takbira ya tatu:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِحَيْنَا وَمَيْتَنَا وَشَاهِدِنَا وَغَائِبَنَا  
وَصَفِيرَنَا وَكَبِيرَنَا وَذَكَرَنَا وَأَنْثَانَا  
اللَّهُمَّ مَنْ أَخْيَيْتَهُ مِنَّا فَاجْعِلْهُ عَلَى الْإِسْلَامِ  
وَمَنْ تَوَقَّيْتَهُ مِنَّا فَتوَفَّهُ عَلَى الْإِيمَانِ  
اللَّهُمَّ لَا تَحْرِمْنَا أَجْرَهُ وَلَا تَفْسِّنَا بَعْدَهُ

**Matamshi:** *Allahummaghfir lihayyina wa mayyitina, wa shaahidina wa ghaibina, wa saghirina wa kabirina, wa dharakina wa unthana. Allahumma, man ahyaitahuu minnaa fa-ahyihii alal-Islam; wa man tawaffaitahuu minnaa fatawaf-fahuu alal-Iman. Allahumma la tahrimna ajrahu wala taftinna ba'dahu.*

**Tafsiri:** E Allah, wasamehe walio hai kati yetu na waliokufa, na waliohudhuria na wasioweza kuhudhuria, na wadogo wetu na wakubwa wetu, na wanaume wetu na wanawake wetu. Ee Allah, usitunyime ujira wake wala usitutie majoribio baada yake. (Ibn Majah, Ktabul Janaiz, Baabud-Dua fis-Salaat alal-janazah).

**Zingatia:** Iwapo maiti ni ya mwanamke msitari wa mwisho wa dua utasomeka:

اللَّهُمَّ لَا تَحْرِمْنَا أَجْرَهَا وَلَا تَفْتَنْنَا بَعْدَهَا

#### DUA KWA AJILI YA MTOTO WA KIUME ALIYEFARIKI

اللَّهُمَّ اجْعَلْنَا لَنَا سَلَفًا وَ فُرُطًا وَ ذُخْرًا وَ أَجْرًا وَ شَافِعًا وَ مُشَفِّعًا

**Matamshi:** *Allahummaj'alhu lana salafan wa faratan, waj'alhu lana ajiran wa dhukhran, waj'alhu lana shafian wa mushaffa-an*

**Tafsiri:** Ee Allah, umfanye mtangulizi wetu, na umjaalie awe ujira na akiba kwetu, na umjaalie kuwa mwenye kutuombea na ambaye maombi yake hupokelewa.

#### DUA KWA MTOTO WA KIKE ALIYEFARIKI

اللَّهُمَّ اجْعَلْنَا لَنَا سَلَفًا وَ فُرُطًا وَ ذُخْرًا وَ أَجْرًا وَ شَافِعًا وَ مُشَفِّعًا

**Matamshi:** *Allahummaj'alha lana salafan wa faratran, wa dhukhran wa ajran, wa shafiatan wa mushaffa-atan.*

**Tafsiri:** Ee Allah, mjaalie awe mtangulizi wetu, na akiba na ujira kwetu, na mwenye kutuombea na mwenye kupokelewa maombi yake.

Baada ya maiti kwisha saliwa tayari, jeneza lipelekwe sasa makaburini ili kuzikwa pasipo kuchelewesha bila sababu yoyote. Jeneza lichukuliwe hadi makaburini mabegani. Waliohudhuria wachukue zamu kwa zamu. kama makaburini ni mbali, maiti inaweza kupelekwa kwa gari. Waliopo hapo wanapaswa kudumu kumkumbuka Allah na kumwombea marehemu msamaha kimoyomoyo.

Kaburi linaweza kuchimbwa kwa kuchimba mwanandani pia ama pasipo mwanandani. Lakini kwa vyovyote, ni muhimu kwamba kaburi liwe pana la kutosha. Kama iko shida fulani, maiti zaidi ya moja huweza kuzikwa katika kaburi moja. kama maiti anazikwa kwa muda tu kwa kunuia kwamba baadaye atazikwa mahali pengine, hapo iko ruhusa kuzika ndani ya sanduku la chuma ama mbao ili mwili usiharibike haraka.

Mwili uteremshwe kaburini kwa uangalifu. Wakati wa kuteremsha maiti kaburini dua ifuatayo yaweza kuombwa:

**بِسْمِ اللَّهِ عَلَى مِلَّةِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ**

**Matamshi:** *Bismillahi, Wabillahi, 'alaa millati Rasulillaahi s.a.w.*

**Tafsiri:** (Twamzika) kwa jina la Allah, na kwa baraka za Allah, juu ya desturi ya Mjumbe wa Allah s.a.w.

Mwili ukiisha lazwa ndani ya kaburi, shuka ya juu ilegezwe kidogo na uso wa maiti ugeuzwe kidogo kuelekea kibla. matofali ama kiunza hutumika kwa kufunika mwana ndani, kisha

mchanga na udongo hujazwa na kufukia kaburi. Wakati huu dua hii yaweza kusomwa:

**بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ مَا حَلَّ لَكُمْ وَمَا لَمْ يَحْلُّ لَكُمْ تَارِثَةٌ أُخْرَى -**

**Matamshi:** *Minha khalaqnaakum wa fihaa nuidukum wa minha nukhrijukum taaratan ukhra.*

**Tafsiri:** Tuliwaumbeni kutoka humo na mle ndani yake Tutawarudisheni na kutoka humo Tutawatoeni mara nyingine.

Ni sawa na desturi ya Mtume s.a.w. kulifanya kaburi liinuke kidogo juu ya ardhi, yaani wakati wa kufukia kaburi mchanga zaidi utiliwe hivi kwamba kaburi liinuke kidogo kama tuta. Baada ya kwisha kuzika tayari mamobi ya pamoja yanaombwa kimoyomoyo na wale waliopo hapo kaburini, kwa kuinua mikono yao ambayo ndiyo maombi ya kumwombea marehemu msamaha. kisha wote wanaondoka hapo wakiomba:

**السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَإِنَّ شَاءَ اللَّهُ بِكُمْ لَلَّا حَقُونَ .**

**Matamshi:** *Assalaamu Alaikum. Wa innaa Insha-Allahu bikum lalaahiquun.*

**Tafsiri:** Salamu iwe kwenu. Nasi Mungu Akijaalia, tutakutana nanyi.

Waliofiwa wapewe mkono wa pole na rambirambi. Ni jambo zuri mno kwamba jamaa wa karibu wa waliofiwa ama majirani wawapelekee waliofiwa chakula cha wakati mmoja kwa uchache.

Haifai kabisa kutenda mambo ya ushirikina. Hali ya msiba na kutoa rambirambi iendelee kwa siku tatu, na baada ya siku tatu maisha yaanze kuwa ya kawaida. Hata hivyo muda wa hali ya msiba kuendelea kwa mjane ni miezi minne na siku kumi sawa

na Quran Tukufu, kwani muda huo ni kwa kumpa nafasi mjane ili apate kutulia kimawazo na kimaono. Sababu yake ni kwamba wanawake katika hali ya kufiwa na waume zao, wanapata tahruki kubwa ya akili kuliko wanaume wanaofiwa na wake zao, na wanapaswa kulindwa na baadhi ya watu ambao wanajichukulia nafasi ya kujifaidisha isiyofaa kwa kuwaonesha wajane huruma zao kwa hila katika hali ya msiba wao mkubwa namna hiyo. Katika muda huo (wa miezi minne na siku kumi) mjane asitoke nyumbani kwake isipokuwa kwa shida yake isiyopeukika. Lakini kama mjane ndiye aliye wa pekee wa kuchuma riziki katika familia wala hawezi kupata ruhusa kutoka kazini kwa muda huo, hapo ye ye anaruhusiwa kwenda kazini, lakini asiwe na mambo mengine isipokuwa kushuhgulikia kazi yake na kisha kurudi nyumbani.

Pia mjane kwa muda huo wa huzuni ajiepushe na kujipamba, kuvaan nguo za shangwe na kutumia rangi midomoni na kadhalika asitumie manukato wala asihudhurie katika sherehe za furaha. Muda wote anapaswa kumkumbuka Allah kwa sabira na kumtolea shukurani Mwumba.

## **ORODHA YA ISTILAHII**

- Adhan: Maneno ya kuwaita Waislamu waje kusali.
- Asr: Sala ya Alasiri inayosaliwa kuanzia wakati wa jua linapoteremka sana hadi kuanza kuzama.
- Ta'awwudh: Maneno maalum ya kumwomba Allah atulinde katika shari ya Shetani.
- Tashahhud: Maneno maalum yanayoombwa kimoyomoyo mwanzoni mwa Qa'dah.
- Dua ya Qunuut:
- Ombi la Kunuut, Dua maalum inayooombwa katika Rakaa ya tatu ya Sala ya witri baada ya kwisha kuinuka katika Rukuu ya mwisho.
- Fajr: Sala ya Alfajiri inayosaliwa wakati wa kupambazuka. Saa zake za mwisho ni wakati linapoanza kuchomoza.
- jua
- Faraidh: Ni wingi wa Fardh.
- Fardh: Maana yake ni faradhi. Neno hili linatumika wakati wa kueleza namna mbalimbali za Sala, ama sehemu mbalimbali za Sala
- Faradhi Kifaya:
- Faradhi yenye kutosheleza. Ni faradhi ya Waislamu wote kwa jumla, ambayo baadhi yao wakitimiza itahesabiwa kana kwamba wote wamekwisha itimiza. kama vile Sala ya maiti
- Fitri: Sadaka inayotolewa na kila Mwislamu kabla hajaenda kusali Sala ya Idil-Fitri.
- Hajj: Kwenda kuhiji Kaaba iliyoko Makkah. Hii ni nguzo ya tano ya Uislamu.
- Idii Adh-ha: Sikukuu ya Kiislamu kwa kukumbuka utii wa Nabii Ibrahimu a.s. na mwanawewe Ismili a.s. ya Allah. Hiyo yaitwa pia Idi kubwa.
- mbele
- Idil Fitri: Idi ndogo. Sikukuu ya Kiislamu inayosherehekewa pindi mwezi wa Ramadhan unapomalizika..

- Imam: Mtu anayewaongoza maamuma katika Sala za pamoja.
- Iqama: Adhana fupi. Ni maneno maalum yanayotam-kwa aaza baada kudokeza kwamba Sala insasa kusaliwa.Isha: Sala ya Isha inasaliwa ya wingu jekundu kupotea. Yaweza kusaliwa hadi usiku wa manane.
- Jilsa: Hali ya kuketi baina ya sujuda mbili.
- Kalima Tayyiba:
- Maneno maalum ya Kiarabu ambayo tafsiri yake ni: hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah; Muhammad ni Mjumbe wa Allah.
- Kalima Shahada: (Pia huitwa Kalima).
- Kutangaza imani ya Kiislamu, yaani kusema: Nashuhudia kwamba hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah. Na ninashuhudia kwamba Muhammad ni Mtumishi wake na mjurid wake.
- Khusuuf: Kupatwa kwa mwezi. Wakati huo Sala maalum inasaliwa inayoitwa Salatul-Khusuuf.
- Maghrib: Sala ya Magharibi inayosalifa wakati jua linapozama hadi wekundu wa jua unapopotea.
- Makruhaat: Mambo yanayohesabiwa kinyume cha heshima na adabu ya Sala.
- Malikii: Ni dhehebu mojawapo la Kislamu.
- Mwadhini: Mwenye kutoa adhana.
- Mustahab: (Wingi wake Mustahabbaat).
- Mambo mazuri ya kupendeza kuhusu Sala.
- Nawafil: Sala za nafali ambazo ni za hiari.
- Niyyat: Maana yake nia.
- Q'a'dah: Hali ya kuketi mwisho wa Rakaa ya pili au ya mwisho ya Sala.
- Rakaa: Manaa yake kukidhi. Yaani kulipa Sala iliyopita.
- Qadha: Kufupisha Sala katika hali ya safari ama hofu.

**Qauma:** Maana yake kuinuka. Ni hali ya kusimama baada ya Rukuu.

**Qiyam:** Hali ya kusimama katika Sala.

**Rakaa:** Sehemu moja ya Sala kuanzia kusimama hadi kusujudia na kadhalika.

**Rukuu:** Kuinama katika Sala kwa kuweka mikono juu ya magoti.

**Sajadah:** (Sujuud):

Hali ya kuanguka kifudifudi katika Sala, yaani kusujudia.

**Salatul-Jumu'ah:**

Sala ya Ijumaa.

**Salat:** Sala. Ni nguzo ya Pili ya Islam.

**Salatul Hajah:** Sala maalum inayosaliwa wakati mtu anapokuwa katika shida kubwa ama ana haja fulani.

**Salatul-Ishraq:** Sala ya nafali inayosaliwa katika vipindi viwili.

**Salatudh-Dhuhaa:**

Kipindi cha pili ya salatul Ishrak.

**Salatut Tasbiih:**

Sala ya nafali ya Rakaa nne inayosaliwa kwa uchache mara moja katika maisha.

**Shia:** Ni dhehebu mojawapo la Islam.

**Sujuud:** Ndiyo sujuda.

**Sujuudus-Sahw:**

Sujuda mbili zinazofanywa kwa kurekebisha kosa lililowahi kutendeka ndani ya Sala pasipo kukusudia, kosa ambalo lingeweza kubatilisha Sala.

**Sunan:** Ni wingi wa neno Sunnat, yaani sunna (Mwendoo Mtume s.a.w.).

**Sunnah au Sunnat:**

Maana yake ni sunna. Ni Sala ambayo umuhimu wake ni baada ya Sala ya faradhi, lakini ni muhimu zaidi kuliko Sala ya nafali.

Sunni:	Ni dhehebu la Islam.
Sura (Surah):	Sura ya Quran Tukufu.
Sutra: Kinga.	Ni kitu kinachowekwa mbele ya mwenye kusali lake. kupitia humo hilo.
	Ni kitu kinachowekwa mbele ya mwenye kusali katika mahali pa wazi kwa kuonesha eneo Mtu mwininge hana ruhusa ya katikaeneo
Tahajjud:	Sala ya nafali inayosaliwa katika sehemu ya mwisho ya usiku kabla ya kupambazuka. Sala hiyo ina thawabu nyingi mno.
Tahmiid:	Maneno maalum ya kumsifu Allah ndani ya Sala baada ya Imam kutamka Tasmii.
Tahmid kwa midia Allah.	jumla ni kumhi-
Takbira Tahrim:	Kutamka Takbira ya kwanza wakati wa kuan- zia ndewe za masikio. tamka Takbira hiyo mtu anakatazwa sasa asizungumze na yejote wala asielekee kulia wala kushoto.
Tarawiih:	Maana yake Tarawehe. Ni Sala maalum inayosaliwa katika mwezi wa ramadhan baada ya Sala ya Isha.